tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



**Wadaiwa kumuua kaka kwa kumpiga na shoka kichwani**

UKURASA 3

UK. 21



**TEN HAG, SANCHO BADO KIZUNGUMKUTI**


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Septemba 17, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581436

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




# MATUMBO JOTO

• **Ni** maofisa wanaodaiwa kutafuna mabilioni, Rais Samia asema anasubiri... *Endelea Ukurasa 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**WANATAALUMA VYUO WAJAZWA MAMILIONI KUCHAPISHA UTAFITI MAJARIDA KIMATAIFA**



SERIKALI imetangaza watafiti 47 kutoka taasisi za elimu ya juu za umma na binafsi ambao wametunukiwa tuzo kwa kuchapisha matokeo ya utafiti...

**UKURASA WA 4**

**MKULIMA, MFUGAJI WAFA KWA RADI WAKISULUHISHWA**

WATU wawili wakazi wa Kitongoji cha Salawe A, Kijiji cha Salawe, Kata ya Ubagwe, Halmashauri ya Ushetu, Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, wamefariki dunia baada ya kupigwa na radi nyumbani kwa mwenyekiti akiwasuluhisha mgogoro uliokuwa...



Mfanyabiashara akiandaa kitoweo cha samaki katika Soko la Kimataifa la Samaki Feri, Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Watoto wanaoumwa sana sasa kuanza kupimwa kisukari

UKURASA 5



MAUAJI YA ANETH

## Mke wa Bilionea Msuya akutwa na kesi ya kujibu

UK. 3

**MICHEZO** YANGA YATAKATA, SIMBA YASHIKWA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Wananchi wa Tandahimba katika Mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa Majaliwa ikiwa ni muendelezo wa ziara yake katika Mikoa ya Kusini. **PICHA:IKULU**

# Wabadhirifu fedha halmashauri matumbo joto

**Na Beatrice Shayo**

MATUMBO joto. Ndiyo hali halisi kwa baadhi ya watumishi wa halmashauri wanaodaiwa kutafuna mabilioni ya shilingi zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye mamlaka hizo za serikali za mitaa.

Hali hiyo inatokana na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa jana katika ziara yake ya kikazi mkoani Mtwara katika moja ya mikutano ya hadhara aliyoifanya jana. Kutokana na kuwapo kwa madai hayo ya ubadhirifu, Rais alisema anasubiri taarifa ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili achukue hatua.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara wilayani Tandahimba, Rais Samia alisema anashangazwa na taarifa ya fedha zinazopelekwa katika halmashauri kuonyesha kutumika vibaya licha ya kuwapo kwa viongozi wa serikali na madiwani.

Rais Samia alisema amemsikia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengewa, akizungumzia fedha nyingi zinazopelekwa katika halmashari na kutumika vibaya badala ya kazi zilizokusudiwa.

"Waziri ameshaeleza TAKUKURU wachukue hatua na mimi ninasubiri taarifa ya TAKUKURU ili tuchukue hatua za juu kabisa. Lakini huwa najiuliza halmashauri hizi zenye madiwani, halmashauri hizi ziko chini ya mkuu wa wilaya, ziko chini ya viongozi wa kamati za siasa za Chama Cha Mapinduzi (CCM), inakuwaje halmashauri inatumia vibaya fedha inakuja kujulikana baadaye?"alihoji.

"Ni kwa nini itumike vibaya? madiwani mko wapi? Kamati za siasa mko wapi? wakuu wa wilaya wako wapi? Kwanini fedha zitumike vibaya? Watu wa TAKUKURU katika hii wilaya wako wapi? Kazi yao ni kuzuia na kupambana, wasisubiri kupambana, waanze na kuzuia rushwa.

"Sielewi kwa nini hali ifike hivi wakati viongozi wote wa serikali wapo hapa. Kwa nini matumizi mabaya yanatokea? Sielewi, ninaomba viongozi chini, mkuu wa mkoa ukae nao mwangalie tatizo liko wapi? Mjirekebishe hasa madiwani mnaosimamia halmashauri mjirekebishe," alisisitiza.

Rais Samia alisema fedha zinazotolewa serikalini haimaanishi serikali ina fedha nyingi bali kwa kuwa imeamua kuwatumikia wananchi kwa kutatua kero zao, ndiyo maana wanazipeleka huko.

"Hizo fedha zinavyoletwa huku zisiwatie kizunguzungu. Fedha zikatumike kwenye yale maeneo yaliyokusudiwa, siwaelewi hii inaonyesha madiwani mmeshindwa kufanya kazi na viongozi wengine mmeshindwa kufanya kazi. Kama hamjashindwa kufanya kazi mngesimamia fedha hizi zitumike vizuri. Hii ni changamoto kwenu, ninaomba mkae na kulirekebisha hilo," alisisitiza.

**RUZUKU ZIONGEZE MAZAO**

Kuhusu ruzuku, Rais Samia alisema akiangalia takwimu za mwaka jana zilizoko mkoani humo, fedha zilizotolewa zilikuwa Sh.bilioni 51.9.

Alisema takwimu za fedha zilizokusanywa za mazao yaani zilizorudi kwa wakulima ni chini ya ruzuku iliyotolewa.

Rais alisema shilingi moja ya ruzuku inatakiwa ikazalishe shilingi tatu hadi tano kwa mkulima kama watakuwa wanachukua ruzuku kubwa na mazao yanayozalishwa lakini kama yanaleta fedha ndogo haina maana.

Samia alisema anafahamu kuna ujanja unaofanywa na wagawaji wa pembejeo kwa kutoa takwimu za uongo na kuwanyima wakulima pembejeo.

"Naomba sana... madiwani na viongozi wa vyama vya ushirika, simameni imara wakulima wapate pembejeo zinazoletwa na serikali ili wazalishe kwa wingi, wakulima na serikali wapate kunufaika. Tumefanya tathmini kwa mwaka jana na mwaka huu mkoa huu (Mtwara) utapatiwa ruzuku za Sh. bilioni 105," alisema.

Kiongozi huyo alisema hakuridhishwa na kiwango cha utekelezaji wa miradi mbalimbali mkoani humo.

Akiwa Nanyamba, Rais Samia alisema serikali imeamua kujenga shule kubwa ya sekondari kwa ajili ya wasichana mkoani humo na kuwataka wazazi na walezi waache watoto wa kike wasome.

"Mkianza kuwashughulikia mapema ina maana hata hii shule ya wasichana iliyojengwa haitapata wanafunzi, watatoka mikoa mingine kuja kusoma hapa," alisema.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| S\NO. | CREDITOR'S NAME | BAIL | TYPE AND PART OF THE GUARANTEE | AUCTIONEER | DATE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HELENA RICHARD MOSHA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KIMARA BUCHA | J&J RECOVERIES | 2-10-2023 |
| 2 | SWEDY H. SWEDY | PAGALE | HATI (OFA) – KIGOGO FRESH | LEGENDS AUCTION MART | 2-10-2023 |
| 3 | PAULINA A. MWANGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – MALAMBA MAWILI | LEHALEL GROUP OF COMPANY LIMITED | 2-10-2023 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

217604802


# Wanataaluma vyuo wajazwa mamilioni kuchapisha utafiti majarida kimataifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza watafiti 47 kutoka taasisi za elimu ya juu za umma na binafsi ambao wametunukiwa tuzo kwa kuchapisha matokeo ya utafiti kwenye majarida ya juu kimataifa ili kuchochea utafiti wa kisayansi nchini.

Katika tuzo hizo, Sh. Milioni 500 zimetolewa na kila chapisho limepata zawadi ya Sh. milioni 50.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza jana jijini hapa kwenye hafla ya utoaji tuzo hizo, alisema machapisho hayo ni kutoka maeneo ya afya, sayansi shirikishi, sayansi asilia na hisabati.

"Hii ni motisha kwa watafiti kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia. Hawa watagawana Sh. milioni 500 kwa vigezo husika. Tunataka wanataaluma wetu wafanye utafiti utakaosaidia kwa maendeleo ya taifa,"alisema.

"Sisi tuna haja ya kuwawezesha wanasayansi wetu katika utafiti kutatua matatizo yetu, tunachokifanya ni kidogo lakini kinatuma salamu, tunataka mtafiti aweze kuchuma maisha yake kutokana na utafiti," aliongeza.

Alisema fedha walizopata zitachagiza kujikita kwenye utafiti wenye tija kwa taifa na kujikwamua kiuchumi.

"Tunataka wajikite kwenye utafiti na si kukimbilia kufuga kuku, kufungua baa ili kupata fedha. Tunataka waende kwenye majarida hayo ili utafiti wao ujiuze na utawezesha kujikwamua kiuchumi,"alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkenda alizindua dirisha dogo la kuwasilisha machapisho hayo yaliyochapishwa ndani ya kipindi cha Julai Mosi, 2022 hadi Mei 31, mwaka huu. Mwisho wa kuwasilisha ni Oktoba 31, mwaka huu.

Alisema katika tuzo hizo yameongezwa maeneo mengine ambayo ni sayansi ya mifugo na kilimo, uhandisi na Tehama.

"Katika mwaka wa fedha 2022/23 bajeti iliyopitishwa ilikuwa Sh. bilioni moja sasa tunafungua tena dirisha ili kuwachukua tuliowaacha ambao wapo ndani ya kipindi hicho ili kufikia kiwango hicho kilichotengwa ambapo hawa tuliowatangaza leo zimetumika Sh. milioni 500," alisema.

Alisema kwa wale ambao machapisho yao yalianza kuchapishwa Juni mosi 2023 dirisha lao litatangazwa baadae.

Mwenyekiti wa Kamati ya Tathmini ya Machapisho Utoaji Tuzo hizo, Prof. Yunus Mgaya, alisema machapisho 82 yalipokewa na kamati hiyo na baada ya mchakato kukamilika machapisho 20 yameshinda.

"Kati yake 10 ni mkondo wa sayansi asilia na hisabati na 10 kutoka mkondo wa afya ya sayansi tiba yamekidhi vigezo vya kupata tuzo na ndani ya machapisho hayo kuna watanzania 47 ambao wamekidhi kupata tuzo hizi kiasi cha Sh. milioni 500,"alisema.

Hata hivyo, alisema kamati hiyo inapendekeza katika tuzo zijazo waombaji wawasilishe wasifu wao na barua ya uthibitisho kutoka taasisi anayofanyia kazi, kufanyika ufafanuzi zaidi kuhusu maeneo ya sayansi yaliyomo ndani ya sayansi asilia.

"Kuwapo na kifungu kinachoainisha adhabu na hatua za kisheria kwa yeyote atakayefanya udanganyifu katika maombi, kuanzisha dirisha mahsusi kwa ajili ya taasisi za utafiti na maendeleo kwa kushirikiana na wizara za kisekta na sekta binafsi. Pia uanzishwe utaratibu wa kutambua mchango wa watafiti mahiri nchini wanaoongoza kwa kuleta fedha za utafiti ili kuendeleza na kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu," alisema.

# HABARI KITAIFA

## Watoto wadaiwa kumuua kaka kwa kumpiga na shoka kichwani

**Na Beatrice Shayo**

WATOTO wenye umri wa miaka 13 na 15, wakazi wa kijiji cha Mbamba, Kilosa mkoani Morogoro wanadaiwa kumuua kaka yao, Wenja Maduka (20), kwa kumpiga shoka kichwani wakati amelala.

Inadaiwa kuwa watoto hao (majina yamehifadhiwa) ambao wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo, walifanya tukio hilo kutokana na vipigo vya mara kwa mara kutoka kwa kaka yao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP) Alex Mkama, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi.

"Hili tukio limetokea Kitongoji cha Ugogoni, Kijiji cha Mbamba. Kijana huyu (inadaiwa) ameuawa kwa kupigwa na shoka kichwani na wadogo zake wawili akiwa kalala,"alisema.

Kamanda Mkama alisema chanzo cha tukio hilo ni kutokana na kuwapo kwa ugomvi wa mara kwa mara. Kaka huyo anadaiwa alikuwa akiwapiga na kuwafanyia vitendo vya unyanyasaji.

"Huwa wanaishi kwa pamoja (wote watatu) kwa kujilea wenyewe. Watoto wameeleza kuwa kaka yao amekuwa akiwapiga na kuwanyanyasa na muda mfupi kabla ya tukio, alitoka kuwachapa na baada ya kufanya hivyo, alikwenda kujilaza kwenye kiduku (nyumba za Wasukuma) iliyoko hapo hapo nyumbani kwao.

"Akiwa amejipumzisha hapo, wadogo zake walikula njama na kwenda kumpiga na shoka kichwani na ndipo alipofariki dunia. Tunawashikilia watoto hawa tukiendelea na uchunguzi," alisema Kamanda Mkama. Alisema wakati tukio hilo likitokea, mama yao alikuwa amekwenda kwenye matibabu kwa mganga na baba yao alishatengana nao. Kamanda alisema baada ya watoto hao kufanya tukio hilo, walimjulisha mama yao kuwa wamempiga kaka yao na amefariki dunia.

"Ndipo mama yao akatoka kwa mganga na alipofika (nyumbani) akakuta mtoto wake amefariki dunia na hawa wadogo wakiwa wamekamatwa na viongozi wa serikali za mitaa na kufikishwa kituo cha polisi," alisema.

Kamanda Mkama ametoa wito kwa wazazi kujikita kwenye malezi mazuri ya watoto wao kwa kuwa roho za kikatili zinatokana na malezi ya hovyo.

"Kama wazazi watajikita katika maadili mazuri ya kuwalea watoto wao hatutegemei kuona matukio kama haya. Wazazi wasikwepe wajibu wao wa kulea watoto wao," alisema.



Mtaalamu wa Afya kutoka Kituo cha Apolo, Swaleh Hassan, akimpima afya mmoja wa wananchi waliojitokeza kupima magonjwa mbalimbali katika kambi maalum ya vipimo na matibabu ya magonjwa yasiyo ambukizwa kama vile macho, presha na saratani ikiwa ni maadhimisho ya kumbukizi ya, Imamu Hussen, katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mke wa Bilionea Msuya akutwa na kesi ya kujibu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imemkuta na kesi ya kujibu aliyekuwa mke wa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, marehemu Erasto Msuya, maarufu kwa jina la Bilionea Msuya, Miriam Mrita, anayetuhumiwa kumuua wifi yake, Aneth.

Mbali na Mrita mshtakiwa mwingine aliyekutwa na kesi ya kujibu ni mfanyabiashara Revocatus Muyela. Wamedai kuwa watapeleka mashahidi na vielelezo kuthibitisha tuhuma hizo dhidi yao na pia watajitetea kwa kiapo.

Uamuzi huo mdogo ulitolewa na Jaji Edwin Kakolaki wa mahakama hiyo, baada ya upande wa mashtaka kufunga kesi kwa mashahidi 25 na vielelezo mbalimbali kikiwamo kisu ambacho kinadaiwa kilitumika kumchinjia Aneth koromeo.

Jaji Kakolaki alisema mahakama baada ya kuzingatia ushahidi na vielelezo vilivyotolewa, imejiridhisha kwamba kuna kesi ya msingi ambayo inawatosheleza washtakiwa wajitetee kama sheria inavyotaka.

"Washtakiwa simameni, kwa mujibu wa kifungu 293 (2) na (a) (b) na cha (3) mahakma inawafahamisha pamoja na haki zenu nilizokwisha waeleza na pia mawakili wenu watawaelewesha kama mtakuwa hamjaelewa vizuri.

"Mnaweza kutoa ushahidi nyie wenyewe au kuita mashahidi ambapo mashahidi wenu wataulizwa maswali kama walivyokuwa wanaulizwa hawa wengine. Pia kuna haki ya kukaa kimya, wakati unatumia haki hii mahakama kuchukulia vinginevyo ambavyo itaona inafaa na kuendelea kutoa uamuzi," alisema Jaji Kakolaki

Washitakiwa hao walizungumza na mawakili wao, Peter Kibatala na Nehemiah Nkoko, walifikia hatua ya kuieleza mahakama hatua ambazo watazitumia.

Mshtakiwa wa kwanza, Mrita alidai kuwa atajitetea kwa kiapo na atakuwa na mashahidi wa kumtetea pamoja na vielelezo. Juzi hakuweza kusema idadi akaomba muda kidogo wa kufanya maandalizi. Muyela alidai kuwa ushahidi wake atautoa kwa kiapo na atakuwa na mashahidi na vielelezo.

"Baada ya kusikia hatua zenu na pia kwa kuzingatia muda wa kikao hiki cha mahakama umefikia kikomo, hatuwezi kuendelea hadi pale Msajili wa Mahakama Kuu atakapopanga kikao kingine, kwa hiyo mtajulishwa.

"Niwashukuru pande zote mbili, watumishi wa mahakama, waandishi wa habari na ndugu na jamaa kwa kuwa na utulivu na kumaliza kiko hiki kwa usalama," alisema

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, alidai kuwa Getruda Mfuru ndiye shahidi wao wa mwisho.

"Tunaiachia mahakama itafakari kama washitakiwa wanakesi ya kujibu au la,"alidai Kimweri

Kibatala na Nkoko kwa upande wao walidai kuwa hawana pingamizi lolote na wanasubiri uamuzi wowote wa mahakama wataupokea.

Mrita ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji ya wifi yake huyo, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni , Dar es Salaam, alikiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.



# Mgombea ubunge Mbarali ajinadi kwa ajenda GN 28

**Na Halfani Chusi**

MGOMBEA wa ubunge Jimbo la Mbarali kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Bahati Ndingo, amesema endapo atashinda atashirikiana na wenzake kusukuma ajenda GN 28 ili kupata ufumbuzi na wananchi kufanya shughuli zao bila wasiwasi.

GN 28 ya mwaka 2008, ni tangazo la serikali la namba 28 la mwaka huo linalowataka wananchi wa Mbarali mkoani Mbeya kutofanya shughuli zozote ikiwamo ujenzi wa makazi na ili kuhifadhi mazingira kutokana sababu za kitaalamu.

Akiomba kura wananchi wa Kata ya Ubaruku, katika mkutano wa hadhara alisema, "Mheshimiwa Mwenyekiti Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Mary Chatanda, shida yetu kubwa ni ardhi," alisema.

Alisema CCM imefanya kazi kubwa ya kuboresha maendeleo ndani ya Mbarali lakini, kilio cha ardhi nimeshafika kwa wajumbe wa Kamati Kuu, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda wakifikishe mbele zaidi.

"Alikuja Pinda na Spika Tulia wakati tunazindua kampeni pale Rujewa nilimwomba, nasubiri majibu. Niliwaambia wamfikishie Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) pamoja na changamoto zilizopo," alisema.

Alisema mwaka jana walizuiwa kulima, lakini tangazo likatoka watu kuendelea na ameomba watoe kibali walime mapema.

Mgombea huyo alisema kuwa suala la GN 28 limekuwa ajenda ya watu fulani (bila kuwataja) ya kufanya upotoshaji huku akieleza kuwa, serikali imelishughulikia.

"Niwaambie wana Mbarali nimeanza kazi hii kabla ya kunipa kura mniamini sitowaungusha," alisema Bahati.

Mbunge wa Makete, Festo Sanga alisema Bahati ni mtu sahihi kuongoza jimbo hilo, akisisitiza watahakikisha wanampa ushirikiano wa kutosha katika utendaji kazi wake ikiwamo suala la GN 28.

"Tukiwa bungeni tutakuwa kama viungo washambuliaji. Nikiwa winga nampasia Bahati akisimama akizungumzia suala ardhi nitasimama na kumuomba Spika kutoa taarifa kuunga mkono anachokisema Bahati.Tutaaungana katika suala hili," alisema.

Chatanda aliwataka wananchi kumchagua mgombea huyo akimsifu kuwa ndiyo mtu sahihi kuziba nafasi ya mbunge aliyepita (Francis Mtega aliyefariki kwa ajali).

# Mkulima, mfugaji wafa kwa radi wakisuluhishwa kwa mwenyekiti

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU wawili wakazi wa Kitongoji cha Salawe A, Kijiji cha Salawe, Kata ya Ubagwe, Halmashauri ya Ushetu, Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, wamefariki dunia baada ya kupigwa na radi nyumbani kwa mwenyekiti akiwasuluhisha mgogoro uliokuwa ukiwakabili.

Tukio hilo limetokea Septemba 11, mwaka huu, nyumbani kwa Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Daniel Malunde, wakati akisuluhisha kesi ya mifugo ya mfugaji Shija Machelewa (57) kuingia shambani kwa mkulima Petro Augustino (62) na kula mazao yake.

Wakati mifugo hiyo ikila mazao ya mkulima huyo, aliyekuwa akiichunga alikuwa ameelekea bondeni kutafuta maji ya kunywa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Janeth Magomi, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema baada ya uchunguzi, miili hiyo ilikabidhiwa kwa ndugu. Hakuna mtu aliyeshikiliwa kutokana na tukio hilo.

Akisimulia namna tukio hilo lilivyotokea, Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Daniel Malunde, alisema siku ya tukio majira ya saa 11 jioni nyumbani kwake akisuluhisha mgogoro huo ndipo radi ilipopiga na kusababisha vifo vya watu hao.

Alisema hivi karibuni alipokea kesi ya mifugo ya Machelewa kuvamia shambani na kula mazao ya mkulima Augustino.

Alisema kesi hiyo ameiendesha kwa siku tatu bila kupata suluhu na mkulima kutaka kulipwa fidia ya mazao yaliyoharibiwa.

Alisema Septemba 11, ikiwa ni awamu ya tatu ya kukutana katika kikao hicho, kila mmoja alikuwa na mashahidi, akiwamo aliyekuwa akichunga mifugo siku ya tukio.

"Kikao kilifanyika chini ya mti wa muembe uliopo kando ya makazi yangu. Wakati tunasuluhisha walitaka hukumu itolewe baada ya kufika shambani kujiridhisha uharibifu uliojitokeza," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema wakati wanajiandaa kuelekea shambani ghafla mvua ilinyesha ndipo walipokubaliana wabaki na waliingia nyumbani kwake.

"Tukaingia ndani. Muda mfupi ilisikika sauti ya radi kubwa. Mimi na mashahidi tukarushwa nje ya nyumba na waliokuwa wakishtakiana wakapigwa na radi na kupoteza maisha papo hapo.

"Tulikuwa saba ndani kwangu tukijikinga mvua iliyokuwa inanyesha majira ya saa 11 jioni ili itakapokatika tuelekee shambani kuangalia uharibifu uliojitokeza kisha tutoe uamuzi wa kesi iliyokuwapo.

"Lakini ilipiga radi kubwa iliyoambatana na mwanga mkali ikatutupa nje, isipokuwa wenye kesi wao walipigwa na kupoteza maisha papo hapo,"alisema.

Malunde alisema shahidi Andrew Masele aliyekuwa upande wa Augustino alijeruhiwa kwa kuwa wakati huo alikuwa karibu na mlalamikaji na alitibiwa Zahanati ya Ilamba na sasa anaendelea vizuri.

Malunde alisema tukio hilo liliwaacha mdomo wazi kwa sababu baada ya radi kupiga liliwaua wale waliokuwa na mgogoro. Watu hawa walizikwa Jumatano.

Diwani wa Ubagwe, Robert Lushesha, alisema wakati tukio hilo linatokea walikuwa katika maziko ya mkulima mwingine, Safari Manjala, aliyejiua kwa bastola shambani kwake.

"Nilipata taarifa za vifo hivi vilivyotokana na radi lakini sikujua kama kulikuwa na kesi ya mifugo kuvamia shamba la mkulima kwa kuwa, kata yangu ni kubwa ina vitongoji 14," alisema.



Mwendesha pikipiki akiwa amepakia viroba vya mkaa akitafuta wateja katika eneo la Kivule jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC aonya abiria wanaotupa taka hovyo

**Na Moshi Lusonzo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameagiza kukamatwa na kuwafikisha mahakamani abiria wa daladala watakaobainika kutupa uchafu nje ya gari.

Akizungumza jana katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika Mbagala Zakhem wilayani Temeke, Chalamila alisema ukamataji huo uhusishe pia, bodaboda wanaopita katika barabara ya mwendokasi.

Chalamila alisema ukamataji kwa wanaotupa taka hovyo utachangia watu kuishi kwa kufuata sheria na kujifunza tabia ya kupenda usafi.

Alisema kuna tabia ambayo imezoeleka kwa abiria wa daladala kutupa taka nje ya gari na kuchangia uchafuzi wa mazingira .

"Utawaona watu kwenye daladala wanatupa uchafu barabarani, hili siyo sawa watu wa aina hii wakamatwe na wachukuliwe hatua ili wajifunze waache tabia ya uchafu," alisema.

Chalamila alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Temeke, mkurugenzi na madiwani kuwa wakali na kuchukua hatua kali kulingana na sheria ndogo za mazingira za halmashauri walizozitunga.

"Tukiwaacha hawa vijana waendesha bodaboda waendelee kutumia barabara ya mwendokasi bila ya kuwachukulia hatua itakuwa tatizo, kuanzia sasa lazima waelewe hawaruhusiwi kupita kweye barabara hiyo," alisisitiza.

Hata hivyo, aliwapongeza viongozi wa wilaya hiyo kwa kudumisha utaratibu wa usafi wa mazingira muda wote na kuwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri ndani ya mkoa huo kwenda kujifunza.

Alisema mafanikio hayo yametokana na viongozi wote na wananchi kujenga umoja na kuaminiana katika utekelezaji wa mipango yao.

Chalamila alisema katika ngazi ya mkoa, wanafanya mazungumzo na wawekezaji kwa ajili ya kujenga mitambo ya uchakataji wa taka na kuwa nishati ya umeme, gesi na mbolea.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mobhare Matinyi, alisema wametumia Sh. bilioni 18 kwa ajili ya kuboresha mifereji mikubwa sita inayokusanya maji taka kutoka sehemu mbalimbali na kuyapeleka baharini.

Alisema suala la usafi limekuwa ajenda yao kuu kwa kuhakikisha kila kata na mitaa inakuwa safi muda wote ili kujiandaa na mvua za El-Nino zinazotarajiwa kuanza mwezi unaokuja.

# Watoto wanaougua sana kupimwa kisukari

**Na Romana Mallya**

DAKTARI wa watoto, Kandi Muze, amesema katika kukabiliana na matatizo ya kisukari aina ya kwanza ambacho huwapata watoto, umewekwa utaratibu wa kuwapima wanaoumwa sana baada ya kufikishwa vituo vya afya.

Akizungumza na Nipashe katika kambi ya siku tatu ya watoto na vijana wanaougua ugonjwa huo iliyofanyika Bagamoyo mkoani Pwani, Dk. Muze alisema takwimu kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) pekee zinaonyesha mwaka 1985 kulikuwa na watoto 35 tu lakini sasa idadi imefikia 400. Alisema wakati kukiwa na ongezeko hilo changamoto iliyopo ni wazazi au walezi kuwafikisha watoto hospitalini wakiwa tayari kwenye hali mbaya.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, mtaalam huyo alisema kwa sasa kuna msisitizo mtoto akipelekwa kituo cha afya kama anaumwa sana, lazima apimwe kisukari.

Alisema hatua hiyo imesaidia kuwatambua na kuwaweka katika mfumo rasmi na kupata dawa na kutibiwa na kwa kiwango kikubwa kukabiliana na madhara ambayo sukari haijatibiwa muda mrefu.

Dk. Muze alisema takwimu kwa idadi ya watoto wenye kisukari aina ya kwanza nchini imefikia takribani 5,000 ambao ndio waliofikishwa kwenye kliniki mbalimbali.

Alisema kwa takwimu za wanaougua ugonjwa wa kisukari nchini imefikia watu 500,000.

Kuhusu kambi hiyo, alisema inaendeshwa chini ya Chama cha Kudhibiti Magonjwa yasiyo ya kuambukiza Tanzania (TANCDA) kwa lengo la kutoa elimu kwa watoto na vijana wanaoishi na kisukari aina ya kwanza, maarufu kama Diabetes type 1.

Daktari huyo alisema wanawapoteza watoto kwa sababu wakati mwingine wanakuwa wanatibiwa matatizo mengine bila kupima sukari yao ikoje.

"Suala la umri, zamani tulikuwa tunaona watoto wameshakua wakubwa wapo katika umri wa balehe kuanzia miaka 10 mpaka 12. Sasa hivi mwelekeo wa walio chini ya umri wa miaka mitano kukipata upo. Tulishampata mwenye umri wa wiki sita," alisema.

Dk. Muze alisema mtoto yeyote mwenye dalili ikiwamo kukojoa sana, kunywa maji mengi kuliko kawaida, kupungua uzito licha ya kwamba anakula kwa wingi, anatakiwa kupimwa ugonjwa huo.

"Kuna aina ya kisukari unaweza kuzaliwa nacho kama umepata kisukari chini ya miezi sita uwezekano mkubwa ni umezaliwa nayo na hii ni aina tofauti kidogo ambacho hupimwa vinasaba na kuna ambayo inaisha na nyingine ya kudumu.

"Na wakati mwingine hutulazimu kupeleka sampuli nje ya nchi kuangalia vinasaba. Kwa watoto wengi hukutwa na aina ya kwanza ya kisukari ambayo huitaji insulin," alifafanua.

Kuhusu kambi iliyowekwa Bagamoyo, mbobezi huyo alisema imehusisha watoto watano wanaotoka kila kliniki Dar es Salaam ambapo pia, kuna wawakilishi wakiwamo wazazi, wauguzi na madaktari.

Alisema lengo ni kuwapangia watoto na wauguzi namna ya kuweka uwiano wa insulin kwa kuangalia kiwango cha sukari cha wakati huo ili kuiweka katika kiwango kinachokubalika.

"Kuangalia ni kwa namna gani wanaweza kula chakula wakashiba lakini sukari ikaendelea kuwa kawaida na kuchomwa insulin," alisema.



Vijana wakitumia usafiri wa baiskeli bila kujali usalama wao katika Barabara ya Nyerere, Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Wazazi wadaiwa kuchangia watoto kubakwa, kulawitiwa

**Na Yasmine Protace**

BAADHI ya wazazi na walezi wanadaiwa kuchangia kukithiri ukatili dhidi ya watoto kwa kuwaachia majukumu ya kuwalea wafanyakazi wao wa ndani na kusababisha kubakwa na kulawitiwa.

Diwani wa Viti Maalum Kata ya Mojohe ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Semeni Mtuka, aliyesema hayo juzi akizungumza na Nipashe kuhusiana na kukithiri kwa vitendo hivyo katika kata hiyo.

"Baadhi ya wazazi huondoka asubuhi kurudi jioni, majukumu huwaachia dada wa kazi (wafanyakazi wa ndani) kuwalea. Unakuta mtoto anafanyiwa ukatili, lakini hana wa kumwambia," alisema.

Mtuka alisema baadhi ya watoto wanafanyiwa vitendo hivyo, lakini wanakaa kimya kwa kuwa wazazi wao hawako karibu nao hadi wanapogundulika baada ya kuharibiwa vibaya na kuathirika kisaikolojia. Akizungumzia kuhusu ukatili uliokithiri kwenye maeneo ya kata hiyo, alisema ni watoto kubakwa, kulawitiwa na vipigo kwa wanandoa.

Alisema katika maeneo hayo, kuna nyumba nyingi ambazo ujenzi wake haujakamilika na kutumika kwa ajili ya kufanyia ukatili huo na udhalilishaji.

Alisema katika vikao na Serikali ya mtaa, wamekuwa wakiwatafuta wenye majengo hayo na kuwaomba kukamilisha ujenzi wa nyumba zao ili kutokomeza vitendo hivyo.

" Majibu yao huwa hawana uwezo wa kujenga kwa kukosa fedha na kusafisha maeneo kwa kufyeka nyasi, lakini baada ya muda zikiota ubakaji na ulawiti watoto unaendelea kufanyika," alisema.

Akizungumzia kuhusu michezo ya kubeti, alisema wamewaomba wanaoendesha kwenye maeneo hayo kuanza jioni badala ya asubuhi ili kudhibiti watoto. " Watoto wengine wanaiba Shilingi 200 ili waende kucheza kamali, wengine ulawitiwa na kupewa pesa ili wacheze mchezo huo," alidai.

Alisema pia kuna watoto wameajiriwa kufanya kazi ya kuchezesha michezo hiyo, ambao wamekuwa wakiwaruhusu wenzao wenye rika lao kushiriki.

Alisema katika vikao vyao vinavyofanyika halmashauri, wameomba michezo hiyo ipelekwe kasino au baa ambako watoto hawaruhusiwi kuingia badala ya kwenye vibanda.

# Dawati la jinsia labisha hodi DIT

**Na Christina Mwakangale**

MRATIBU wa Madawati ya Jinsia Taasisi za Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Gift Msowoya, amezindua Dawati la Jinsia katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), ili kushughulikia ukatili dhidi ya wanafunzi na watumishi.

Msowoya alisema dawati hilo lilizinduliwa hivi karibuni jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kupokea taarifa kuhusiana na vitendo hivyo katika taasisi hiyo.

"Mnapaswa kuwa na ofisi yenye usiri itakayomfanya mtu yeyote kutoa taarifa za ukatili bila woga, muwe pia na namba ya simu ili kupokea taarifa za ukatili wakati wowote," alisema Msowoya.

Alisema taasisi hiyo inapaswa kuunda klabu za ukatili wa jinsia ya wanafunzi ili kusaidia upatikanaji wa taarifa na kutolifanya dawati hilo kuwa la watu binafsi. Pia Aliitaka DIT kutenga bajeti kwa ajili ya dawati hilo na kutoa taarifa kila robo tatu ya mwaka.

"Dawati lisiwe kwa ajili ya kuangamiza watumishi na wanafunzi bali mfuate sheria na taratibu zilizowekwa kila mtumishi afanye kazi yake au masomo kwa kufuata taratibu.

"Utandawazi umekuwa changamoto kubwa kwa wanafunzi wengi kuingiwa tamaa na kujikuta wakifanyiwa vitendo vya ukatili, muwasaidie kubadili mitazamo yao wasione maisha rahisi kwani mwisho wake ni mbaya."

Msowoya alisisitiza kuwa dawati hilo linapaswa kusaidia kukinyanyua kizazi cha sasa ili kiweze kujitambua na kuiokoa nchi kufikia dira ya dunia ya maendeleo kukabiliana na vitendo vya ukatili.

Naibu Mkuu wa Taasisi Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu DIT, Prof. Ezekiel Amri, alisema uzinduzi wa dawati hilo pamoja na uwapo wa sera, utaongeza chachu na ufanisi wa taifa kukabiliana na vitendo hivyo.

Prof. Amri alisema kupitia dawati hilo, wamelenga kutoa elimu ya ukatili wa jinsia kwa wafanyakazi, wanafunzi na watoa huduma wa taasisi na kuendesha semina ili kudhibiti vitendo hivyo.

Alisema wataweka utaratibu kutoa elimu dhidi ya vitendo hivyo, kutoa takwimu, kuainisha matatizo na kuweka mazingira rafiki ya usawa wa jinsia kwa wanafunzi na wafanyakazi,

Mratibu wa Kitengo cha Jinsia, Mary Kidima alisema ukatili wa kijinsia una tabia ya kujirudia, hivyo haipaswi kuvumiliwa na kuwataka watu wanaofanyiwa vitendo hivyo watoe taarifa mapema ili kushughulikiwa kwa wakati. Alizitaja changamoto zinazokwamisha juhudi za taasisi hiyo kufikia malengo kuwa ni uelewa mdogo wa baadhi ya wanajamii kuhusu dawati hilo kutokana na imani potofu kuwa linalenga kutetea wanawake na limekaa kiharakati.

" Ukatili wa kijinsia unaweza kufanywa na yeyote mwanaume dhidi ya mwanamke au mwanamke dhidi ya mwanaume, ndio maana dawati linashughulika na jinsia zote. Wahanga wengi wa ukatili wa kijinsia ni waoga wa kutoa taarifa na hata ushahidi pale inapohitajika hivyo tatizo linaendelea kukua bila wahusika kuchukuliwa hatua yoyote," alisisitiza Kidima.

Kaulimbiu ya uzinduzi huo ni Vunja Ukimya, Fichua Ukatili wa Kijinsia' ikitoa wito kwa wanajamii kutofumbia macho vitendo hivyo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mipango madhubuti ifanyike kupunguza foleni barabarani

**KATIKA** moja ya Habari zilizobeba uzito wa juu kwenye gazeti hili ni kuwapo kwa hasara kubwa katika mkoa wa Dar es Salaam kutokana na msongamano wa magari wakati wa kwenda kwenye shughuli za uzalishaji na kurejea nyumbani.

Kamishna wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), David Kafulila, alisema kutokana na hali hiyo, mkoa umekuwa ukipoteza wastani wa Sh. Trilioni 1.4 kwa mwaka. Alitolea mfano kwamba katika sehemu ya kutumia dakika 10, mtu anatumia dakika 50 kufika mahali anakokusudia kwenda, jambo ambalo linawafanya watu wengi kuchelewa katika shughuli za uzalishaji.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali ili kupunguza msongamano wa magari.

Kuhusu mkakati wa serikali kupunguza foleni, alisema kwa sasa serikali inaangalia namna ya kualika wawekezaji katika reli ya Dar es Salaam ili kujenga barabara za kutoa watu katikati ya jiji na zile zinazoingia na kutoka. Kukamilika kwa mpango huo, kutaokoa upotevu wa fedha.

Kauli ya Kafulila kuhusu msongamano wa magari barabarani hususan asubuhi na jioni si ngeni. Jambo hilo limekuwa likizungumzwa mara kwa mara na hata ikaanzishwa mipango ya kupunguza tatizo hilo.

Moja ya njia zilizobuniwa ni kuwapo kwa usafiri wa treni kutoka Stesheni hadi Mabibo na nyingine kutoka Pugu hadi Stesheni, maarufu kama 'Treni ya Mwakyembe'. Njia nyingine ambayo ilianzishwa mahususi kupunguza tatizo hilo ni kuwapo kwa usafiri wa Mwendokasi kutoka Kimara hadi Kivukoni, Gerezani na Kinondoni Morocco.

Kwa ujumla hali hiyo imesaidia kwa kiasi kupunguza tatizo la msongamano wa magari barabarani kwa sababu njia hizo zinafanya watu wasafiri kwa muda mfupi na kuwahi kwenye maeneo yao ya kazi pamoja na nyakati za jioni wakati wa kurejea kwenye makazi yao.

Jitihada zaidi zinaendelea kwa kujenga miundombinu ya mwendokasi hadi kufika maeneo ya Mbagala na Gongo la Mboto. Kukamilika kwa ujenzi huo kutawezesha usafiri katika maeneo hayo ambayo yana wakazi wengi, kuleta unafuu wa usafiri na kupunguza hasara inayopatikana kila mwaka.

Ni imani kwamba miundombinu mingine ya mwendokasi kama itajengwa kutoka Tabata relini Mbezi Mwisho kupita Kinyerezi, Buguruni, Mwenge na Tegeta hadi Kinondoni Morocco, pia itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza adha hiyo.

Hata hivyo, ni jambo la faraja kuwapo kwa taarifa kwamba serikali imealika wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Dar es Salaam ambayo pia itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la msongamano wa magari na kurahisisha usafiri kwa wakazi wa mkoa huo.

Pamoja na hayo, serikali kuu kwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa katika mkoa, inapaswa kufikiria ujenzi wa madaraja ya juu kama ilivyofanyika Ubungo, TAZARA. Chuo cha Uhasibu na kona ya Barabara ya Nyerere na Chang'ombe ambayo yamerahisisha usafiri kwa wanaotumia njia hizo. Wengi wanakumbuka adha walizokuwa wanapata wananchi kutokana na hali ngumu ya usafiri katika maeneo hayo lakini baada ya kuwapo kwa miundombinu hiyo, kumekuwa na unafuu mkubwa.

Kutokana na miundombinu hiyo kusaidia kupunguza adha hiyo, ni wakati sasa wa kuangalia namna ya kujenga madaraja na barabara za kupishana katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam pamoja na njia za pembeni ili kupunguza adha ya wananchi kutumia muda mwingi barabarani badala ya kujikita katika uzalishaji mali, kuinua uchumi wao na kuchangia pato la taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wanasiasa zingatieni wito huu wa Rais Samia

**MIKUTANO** ya hadhara ya vyama vya siasa inaendelea kutikisa maeneo mbalimbali nchini tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipoondoa zuio la mikutano la kutokuwapo kwa mikutano hiyo Januari, mwaka huu.

Hata hivyo, baada ya kuondoa zuio hilo lililokuwa limedumu kwa zaidi ya miaka mitano, kumejitokeza sintofahamu kutokana na baadhi ya wanasiasa kutumia uhuru wa kutoa maoni kwa maneno yenye ukakasi.

Kitendo hicho kimemfanya Rais Samia awakumbushe wanasiasa kuwa hakuna uhuru usio na mipaka, na kwamba mipaka si ya kisheria, hata kibinadamu na kuwataka wazingatie hilo.

Binafsi ninaunga mkono kauli hiyo, kwani siasa za kistaarabu ni moja ya misingi muhimu ya amani kwenye taifa lolote, hivyo ingekuwa ni vyema wananchi, wanasiasa na viongozi wakakosoana kwa staha.

Wajibizane kwa staha na penye kusifia au kushauri wasifie na kushauri. Jambo la kuzingatia liwe ni kuchunga ndimi, ili kuepuka siasa za majitaka ambazo zinaweza kusababisha watu wakachukiana.

Ni vyema wanasiasa wakavumiliana na kuheshimiana, huku wanachama wa vyama vya siasa kila mmoja aone umuhimu wa mwanachama mwenzake ambaye ni chama kingine.

Kwa njia hiyo, ninaamini itakuwa ni rahisi chama cha siasa kufikisha ujumbe wake vizuri kwa wananchi badala ya kutumia maneno yenye ukasisi ambayo yanaweza kuwakera hata wale wanaohutubiwa.

Nafasi hiyo ya kutoka kwenye kifungo cha zaidi ya miaka mitano, ingekuwa ni fursa kwa vyama vya siasa kuelezea sera ili kujipatia wananchama zaidi wanaoridhika na sera za vyama hivyo.

Iwapo vitaendelea kutumia maneno yenye ukakasi katika kufikisha ujumbe kwa wananchi, ninadhani inaweza kuwa vigumu kushawishi wananchi badala yake watakaofurahia ni wale wanaopenda lugha hiyo.

Chama cha siasa kujijenga kwa wananchi ni jambo la muhimu ili kupata wafuasi na wanachama wengi zaidi wa kukiunga mkono wakati wa uchaguzi kwa ajili ya kushika dola.

Njia hiyo pia inasaidia kuwafanya wanasiasa wote bila kujali itikadi za vyama vyao, kusimamia amani, mshikamano na umoja kwa maslahi ya taifa mapana ya umma wa Watanzania. Kinyume na hapo, itakuwa ni sawa na kufanya siasa za majitaka.

Suala la kutofautiana mtazamo, maoni na utendaji, ni jambo la kawaida, bado wanasiasa wanaweza kutumia lugha nzuri kukosoana ili hatimaye kufikia uamuzi wa pamoja, kwa sababu wote wanajenga nchi moja ambayo ni Tanzania, hivyo si vyema kugombania fito.

Licha yna tofauti zinazotokana na itikadi za vyama, bado wanasiasa ni Watanzania ambao kwa namna moja au nyingine wanahitajiana, ili kuijenga mama Tanzania yenye watu wanaoheshimiana na kuthaminiana.

Kwa wanasisa wenye kiu ya dhati ya kutaka kuomba ridhaa ya kuongoza nchini, ni vyema wakawa makini na kuchukua tahadhari hasa katika mipango yao, kauli zao na matendo yao, ili wasiwe sababu ya kuchochea ya kulalamikiwa kwa maneno yenye uakakasi wanayotoa wanapokosoa.

Ninaamini wanasiasa wote wameshuhudia uthubutu wa Rais Samia kuondoa zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa ili vyama hivyo viweze kustawi kwa kujiongezea wanachama zaidi.

Lakini ruhusa hiyo inapotumika ndivyo sivyo, ninadhani sio sahihi. Rais naye ni binadamu kama wengine, anaweza kukosea, anaweza kukosolewa, ila ukosoaji usingefaa kutweza utu wake.

Mwenyewe ametoa ruhusa ya kukosolewa lengo likiwa ni kusaidia kujenga nchi, hivyo uhuru huo wa kutoa maoni, kushauri na kukosoa visingefaa kumfanya kama hafai mbele ya umma wa Watanzania.

## FIKRA MBADALA

# Wananchi ndio wenye Katiba



Pascal Mayalla

LEO naendelea na makala elimishi kuhusu Katiba yetu ya mwaka 1977 kwa jicho la mtunga Katiba. Wiki iliyopita tuliishia jinsi aliyekuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Democratic Party (DP), Mchungaji Christopher Mtikila (Mungu amuweke mahala pema peponi) mwaka 1993 alifungua kesi No. 5 ya mwaka 1993.

Mchungaji Mtikila alifanya juhudi kubwa kukipinga kifungu hiki na Mahakama Kuu kupitia kwa Jaji Kahwa Lugakingira (Mungu amweke mahala pema peponi), ikatamka wazi na bayana kuwa kipengele hicho ni batili na kinakiuka katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ya mwaka 1977, hivyo kifutwe na kutoa haki kwa kila Mtanzania kuwa na haki ya kushiriki kugombea uongozi wowote ndani ya nchi.

Baada tu ya Mtikila kushinda kesi, serikali ilifanya mambo mawili makubwa ya ajabu! Kwanza ilikata rufani. Hivi kwa uamuzi kama huu, serikali ilikata rufani kwa maslahi ya nani?

Wiki iliyopita nilisema ile Ibara ya 64(5) inayotamka Katiba ni sheria mama, sheria nyingine yoyote inayokwenda kinyume cha Katiba ni batili, aliyebatilisha sheria batili ni katiba yenyewe na si Mahakama! Kazi ya Mahakama ni kutamka tu huo ubatili na baada ya tamko hilo, sheria hiyo inakuwa tayari ni imebatilika. Unawezaje kukata rufani kwa kitu kilichobatilishwa na Katiba?. Kiukweli kabisa hili ni jambo la ajabu sana.

Jambo la pili la ajabu sana na kubwa ya mwaka ni serikali yetu ilipeleka bungeni kwa hati ya dharura, Sheria Na. 34 ya mwaka 1994, kufanya marekebisho ya nane ya Katiba ya JMT na kukichomeka kipengele hicho ndani ya katiba, hivyo kuibatilisha ile hukumu ya Jaji Lugakingira! Hapa ndipo hoja inapoanzia katika siasa zetu kwa serikali kufanya kazi kwa maslahi ya kisiasa ya watu fulani na chama fulani, hivyo kupoteza haki ya wengi kwa ajili ya kuwanufaisha wachache..

Hiki kilichofanyika, mimi nakiita ni kitendo cha kihuni! Watanzania tulifanyiwa uhuni na serikali yetu kwa kuinajisi Katiba yetu. Kitu kimeelezwa ni kinyume cha Katiba, kinatoa haki zilizotolewa na Katiba, halafu serikali hiyo hiyo inakuja kuihalalisha haramu hiyo kwa kuiingiza rasmi kwenye Katiba!

Mchungaji Mtikila, licha ya kuwa ni mwanasiasa, alikuwa ni mtu wa Mungu kiukweli kabisa kwa sababu hakukubali kabisa Katiba yetu inajisiwe, hivyo akafungua kesi nyingine No. 10 ya mwaka 2009 kupinga marekebisho hayo ya nane ya Katiba na kuyaita ni ubatili.

Katika kesi hiyo, Mchungaji Mtikila aliomba mambo mawili makuu ambayo ni;-

*Mahakama itamke ibara 39 na 67 za katiba zilizorekebishwa na marekebisho ya 8 kwa Sheria Na. 34 ya mwaka 1994 ni batili na kinyume cha Katiba.

*Kutamka wazi kuwa kila Mtanzania ana haki ya kugombea kwa mujibu wa Ibara ya 21 ya Katiba bila kulazimishwa kudhaminiwa na chama cha siasa, hivyo mtu anaweza kugombea kama mgombea binafsi.

Mahakama Kuu chini ya majaji watatu (majaji watatu kisheria inaitwa Half Bench) Jaji Amir Manento, Salum Masati na Thomas Mihayo, wakayakubali mambo yote mawili ya Mchungaji Mtikila na kumpa ushindi tena kwa kutamka marekebisho hayo ya 8 ya katiba ni batili.

Serikali yetu ya wakati huo, ilikata tena rufani na safari hii Mahakama Kuu ikakaa 'Full Bench' ya majaji saba chini ya aliyekuwa Jaji Mkuu Agustino Ramadhani, akisaidiwa na majaji Eusebia Munuo, January Msoffe, Natalia Kimaro, Kassim Mbarouk, Benard Luanda na Sauda Mjasir. Jopo hilo la majaji, Juni 17, 2010 lilitoa hukumu ya ajabu kabisa kutokea Tanzania.

Mahakama ya Rufani katika suala hilo haikuwa peke yake bali iliwaita mabingwa wabobezi na wabobevu wa sheria na Katiba kuisaidia. Hawa wanaitwa marafiki wa mahakama, kwa Kiingereza ni 'friends of the court', kisheria wanaitwa 'Amicus Curiae', ambao ni Othman Masoud Othman, Prof. Palamagamba Kabudi na Prof. Jwan Mwaikusa (Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi).

Uamuzi wa Mahakama ya Rufani uliamua kitu cha ajabu sana na hapa nanukuu: "So as to let the will of the people prevail as to whether or not such (independent) candidates are suitable. We are definite that the courts are not the custodian of the will of the people. That is the property of elected Members of Parliament."

Kwa ujumla hii ni kauli ya ajabu sana kutolewa na mahakama yetu kwenye jambo zito na muhimu kama hili. Kitendo cha Mahakama kujivua jukumu la kuwa 'the custodian of the will of the people' ni kitendo cha ajabu na kushangaza.

Kama Katiba imetoa haki fulani, kitendo cha Bunge kutunga sheria ya ajabu kabisa kuifuta haki hiyo, kinyume cha Katiba ni mhimili wa Bunge kujiinua juu ya Katiba.

Kitendo cha Mahakama kutamka haiwezi kuliingilia Bunge lililovunja Katiba, ni kutotimiza majukumu yake ya kimhimili kilamilifu kwa kutotimiza jukumu la 'checks and balances'

Mahakama ya Rufani ikaamua kuwa Mahakama haina mamlaka ya kuliingilia Bunge, katika vipengele vya Katiba, kumaanisha kwa vile marekebisho hayo ya 8 yamefanywa na Bunge, hivyo ni Bunge ndilo lirekebishe kipengele hicho! Kwa maoni yangu, uamuzi huu si utii wa mhimili wa Mahakama kwa mhimili Bunge, bali huu ni ukondoo wa hali ya juu. Sheria batili bado imo kwenye sheria zetu na kipengele batili hicho bado kimo ndani ya Katiba yetu.

Uchaguzi wa mwaka 2015 ukalithibitisha hili, kumbe badhi ya majaji wetu ni makada!, Jaji Mkuu Mstaafu aliyeongoza jopo hilo, alichukua fomu kugombea urais. Baadhi ya wale marafiki wa mahakama, tunawajua na tunawaona na ukada wao. Unategemea nini kama sheria za nchi hii zitafinyangwa finyangwa kwa manufaa ya wachache?

Katiba ilisema kila Mtanzania ana haki ya kushiriki uongozi. Hili sharti la kudhaminiwa na chama lilitoka wapi na kwa kwa nini watu walazimishwe kuwa wanachama wa vyama ili wadhaminiwe, ndipo wagombea?. Kama mtu ana uwezo wa kuwatumikia wananchi wa eneo lake na kuwaletea maendeleo bila kupitia chama chochote, kwa nini azuiwe?

0754 270403

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Muswada wa wenza si rafiki kwa Watanzania



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

KUNA mtu nilimsikia siku moja akisema hakika Watanzania tutafika mbinguni tumechoka kisawasawa. Nilipomwuliza kisa nini, akaniambia ni mambo yanayotusonga kila kukicha.

Akaanza na suala la mkataba wa serikali ya Tanzania na Dubai kuhusu kampuni ya Dubai Port World kwamba umewagawa wananchi pande mbili na hata kujenga ubaguzi miongoni mwao.

Iko kambi ambayo imeshikilia kuwa mkataba ni mzuri na una nia njema ya kuijenga nchi kupitia uwekezaji bandarini lakini wako wanaoupinga wakidai kuwa wanakuja kumilikishwa raslimali za nchi hii na sisi kubaki watupu.

Akasema watu wamebishana na kujadiliana wee na hatimaye kuishia kugawanyika na kujengeana chuki, huku wanaokujia kuwekeza wakikaa kimya na kuangalia vita vya panzi.

Lakini kabla hili halijaisha huku kukiwa na mjadala mwingine kuhusu Katiba mpya, akaibuka kigogo mmoja wa Serikali, akasema Katiba haiwezi kupatikana bila kwanza Watanzania kupata elimu ya miaka mitatu.

Mwananchi mmoja akatoa macho aliposikia hayo, akajiuliza Watanzania hao wataelimishwa vipi kwa miaka mitatu kana kwamba huko nyuma hakukuwahi kuwa na elimu ya Katiba chini ya Mzee Joseph Warioba?

Akahoji tena, hivi kama Watanzania walishindwa kuijua Katiba kwa miaka zaidi ya 60, leo hiyo miaka mitatu watаijua kwa walimu wapi ambao hatukuwa nao nchini kwa kipindi chote hicho?

Kabla upepo wa mabishano ya mkataba na Katiba haujatulia, sasa umekuja muswada mwingine wa kutaka wake na waume wa viongozi wakuu wastaafu wa nchi, eti nao walipwe mafao ya kustaafu yanayotokana na ajira za wenzi wao hao!

Hivi sasa mjadala umehamia huko, vichwa vitauma mpaka tukome kwa kweli. Muswada unapendekeza mwenza wa Rais mstaafu aibuke na asilimia 25 ya jumla ya mshahara wa mwenzake alipokuwa kazini, familia ya Rais mstaafu kila mwezi ipate asilimia 60 ya mshahara wa Rais aliye madarakani. Hivi jamani hebu tuiangalie Tanzania, nchi masikini yenye mafukara wengi na watu wachache wenye ukwasi kufuru. Badala ya kuangalia watu wenye hali duni wakainuliwa, tunataka kutumia falsafa ya mwenye nacho aongezwe na asiye nacho anyang'anywe hata kidogo alichonacho. Kweli?

Hivi mke au mume wa Rais, Makamu wa Rais au Waziri Mkuu anaishi maisha magumu kiasi cha mumewe au mkewe akistaafu basi alipwe naye mafao jamani? Hivi tunamwangalia mama au baba wa kijijini mwenye maisha yaliyosawajika kweli?

Huku ni sawa na kutaka kubeza wananchi wa vijijini, kwamba hawana maana yoyote na kwamba ni bora wafe na umasikini wao, lakini wakiendelea kuzalisha kwa maslahi ya matajiri na viongozi walioko mijini.

Tulidhani Serikali ingekuwa na muswada wa kuangalia masikini na vijana wasio na ajira wanasaidiwaje, kuliko kutaka kuwaongeza ulaji viongozi na familia zao. Na pengine haya ndiyo hufanya watu kutaka kuuana wakiwania nafasi za juu za uteuzi au uchaguzi.

Itashangaza sana kuona wabunge wakiupitisha muswada huu kuwa sheria, eti itumike kwa ajili ya kunufaisha wake na waume wa viongozi ambao kwa sasa wanapokea mishahara minono na marupurupu, achilia mbali vyombo na watumishi, vinavyowawezesha kuweka akiba watakayokula na kuhudumiwa vizuri mpaka kifo. Hivi sasa mathalan, vijana wengi wanamaliza masomo yao ya juu hata vyuo vikuu, wanaranda mitaani na shahada zao, wakisaka ajira huku wakipigwa na siasa za 'jiajirini', bila hata kuwa na mitaji, kumbe mitaji inapangwa kupewa wake na waume wa viongozi wastaafu. Hii ikipita, kidogo kidogo tutasikia hata wajane na wagane wa wabunge nao wanastahili walipwe mafao mpaka kufa, kutokana na mchango wa waume au wake zao walipokuwa wabunge.

Na ikipita ya aina hii, bila shaka sasa kugombea ubunge itakuwa vita kwani itakuwa tayari inajulikana tu, kuwa nikisha kuwa mke au mume, mjane au mgane wa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waziri na Mbunge, mafao yatanihusu.

Uzuri wa Watanzania ni watu rahim, haya yote yatapita, kwani wamezoea kumwachia Mungu awaamulie huku wakiendelea kuumia, Dipiwelidi itakuja itafanya yake, Katiba itakuja lakini baada ya kuisomea miaka mitatu kama shahada na mafao ya wenza wa vigogo yatakuja.

Tufikirie Watanzania masikini wanaoteseka na watoto wao, badala ya kujitafakari sisi wenyewe hususan wakubwa na kujirundikia mapesa ambayo hata hatutayatumia kwa raha, kwani yatakuwa yanalaaniwa na vilio vya masikini wa nchi hii. Tumeshindwa kupambana na maadui wa msingi, ujinga, umasikini na maradhi sasa tunapambana na wananchi wetu wenyewe kwa kujifikiria na kujipendelea bila sababu yoyote, huku tukijua baadhi ya wenza waliwekeza wakati wenza wao wakiwa kileleni na uwekezaji wao bado upo. Sasa tunataka kuwaongeza nini na kwa sababu ipi?

Huu muswada uachwe tutatue matatizo ya wananchi wetu kwanza, na kama kutakuwa na salio la fedha basi tuzigawane Watanzania wote kama tulivyotaka kugawiwa zile Toyota Noah zilizoyeyuka na makinikia! Lazima tufike mbinguni hoi kabisa. Alamsiki!

# Mbaroni madai kumtoa mwanafunzi ujauzito

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani hapa, linamshikilia muuza duka la dawa za binadamu, Pendo Maduhu, Mkazi wa Lyabukande kwa tuhuma za kumtoa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne kwa kutumia vidonge na kuhatarisha maisha yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema juzi kuwa pia wanamshikilia mwanaume anayedaiwa kumpa ujauzito mwanafunzi huyo, Nzengo Madulu.

Kamanda Magomi alisema kuwa muuza duka huyo anadaiwa kumtoa ujauzito mwanafunzi huyo Septemba 12, mwaka huu majira ya saa nne usiku.

Alisema mwanafunzi huyo ambaye (jina lake limehifadhiwa) baada ya hali yake kuwa mbaya alikimbizwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga na kwamba anaendelea kupatiwa matibabu chini ya ulinzi wa Polisi.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga tunamshikilia muuza duka la dawa za binadamu, Pendo Maduhu na mtia mimba Nzengo Madulu, wakazi wa Lyabukande wilayani Shinyanga, baada ya kuhatarisha maisha ya mwanafunzi, mmoja akituhumiwa kumpatia ujauzito na mwingine kumtolea na kuhatarisha maisha yake,"alisema Magomi.

Alisema baada ya mwanafunzi kumeza dawa hizo za kutoa mimba (jina la dawa linahifadhiwa), alijisikia kwenda haja na alipofika chooni alitoa mtoto ambaye hajakamilika.

Alisema upelelezi utakapokamilika watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayowakabili.

Alitoa wito kwa wanafunzi kuacha kujiinguiza kwenye mahusiano ya mapenzi wakiwa katika umri mdogo badala yake wasome na kutumiza ndoto zao.

Pia aliwaomba viongozi wa dini na mashirika mbalimbali mkoani hapa ndelee kutoa elimu ya kupinga kuendelea kutoa elimu dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na jeshi hilo ili watoto wa kike wabaki kuwa salama, wasome na kutimiza malengo yao.

# Mstaafu adaiwa kuuawa na mpangaji akidai kodi

**Na Steven William,** MUHEZA

MKAZI wa Michungwani, Muheza mkoani Tanga, John Hiza, anadaiwa kufariki dunia baada ya kupigwa kichwani na kufa na mpangaji wake, John Mwangowela, wakati akidai kodi katika nyumba yake.

Hiza (71) ambaye ni ofisa mstaafu wa kitengo cha maabara katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadam (NIMR) Kituo cha Muheza, alifariki dunia Jumatano wiki hii nyumbani kwake katika mtaa wa Sige Gesti , Michungwani katika kitongoji cha Genge wilayani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi, alisema juzi kuwa Hiza alikuwa anamdai mpangaji wake kodi ya miezi mitatu.

Alisema baada ya kufika nyumbani alimtaka mpangaji kumlipa kodi ya pango, ndipo ugomvi ulipoanza na Mwangowela kumpiga hatimaye kumsababishia kifo.

Alisema mwenye nyumba na mpangaji wake baada ya kurudi nyumbani jioni kutoka katika matembezi yao eneo la Genge, walianza kuzozana kuhusu kodi na nyumba aliamua kutia gundi kali (super glue) kufuri ili mpangaji asiingie ndani kwa kuwa anamdai kodi ya pango.

Kutokana na kitendo hicho, kamanda alisema mpangaji huyo alionyesha kukerwa na hatimaye kumshushia kipigo mwenye nyumba kichwani kwa kutumia gongo la mti na jiwe, hivyo kumsababishia mauti.

Jirani wa eneo hilo, Ally Mohamed, alisema mtuhumiwa huyo alitekeleza mauaji hayo ya mwenye nyumba wake majira ya saa 1:00 usiku kwa kumpiga na gongo la mti na jiwe kichwani kisha kuanguka na kupoteza maisha.

Alisema baada ya mpangaji huyo kufanya tukio hilo, alitaka kutoroka ndipo mpangaji wa chumba cha, Pili Saidi, alipopiga kelele na majirani wakiwamo watu wa usalama, walifika na kumkamata kisha kumfikisha kituo kikuu cha polisi cha Muheza mjini.

Kwa sasa, mtuhumiwa anashikiliwa katika kituo cha polisi cha Mang'enya wilayani Muheza kwa mahojiano zaidi kabla yah atua zingine za kisheria kuchukuliwa.

Mke wa marehemu, Theresia Francis, alisema ameishi maisha ya ndoa na mume wake huyo na kubarikiwa kuwa na watoto sita.

Elia Mdimu, ambae ni ndugu wa karibu wa marehemu, alisema mazishi ya ndugu yake huyo yalitarajiwa kufanyika jana katika kijiji cha Bombani baada ya shughuli za kuuaga mwili kukamilika huko Michungwani, Muheza.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, akiburudika na baadhi ya walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini na wananchi wa Mtaa wa Mbiti Kata ya Mhanga, Bariadi mkoani Simiyu baada ya kukagua nyumba ya mtumishi ya zahanati ya Mbiti iliyojengwa kwa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) juzi.**PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Kikwete akunwa utekelezaji miradi TASAF

**Na Lusungu Helela,** BARIADI

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, ameeleza kuridhishwa na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mkoani Simiyu.

Kutokana na kuridhishwa huko, amezitaka halmashauri zote nchini zinazotekeleza miradi ya maendeleo hususani kwenye sekta ya huduma za jamii, kujifunza kutoka mkoa wa Simiyu ambako kuna mafanikio makubwa.

Naibu Waziri Kikwete ameyasema hayo juzi mjini hapa baada ya kupokea ripoti ya utelekezaji wa miradi ya TASAF katika mkoa wa Simiyu ambao pia ni miongoni mwa mikoa mitano inayotekeleza kwa majaribio miradi ya kupunguza umaskini awamu ya nne (TPRP IV).

"Simiyu ni moja ya mikoa ya mfano kwa utekelezaji na usimamizi mzuri wa miradi ya TASAF. Nimeridhishwa sana na hatua kubwa iliyopigwa katika utelekezaji wa shughuli hizi ambazo zina lengo la kuondoa umaskini na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii," alisema.

Aidha, Kikwete alisisitiza umuhimu wa waratibu na wasimamizi wa miradi ya TASAF kuendelea na ufuatiliaji wa karibu wakati wote wa utekelezaji ili kuhakikisha miradi yote inaendana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Katika hatua nyingine, Kikwete alisema serikali kupitia TASAF imesitisha uhawilishaji fedha kwa walengwa kwa njia ya mitandao ya simu na badala yake kazi hiyo itafanyika kwa njia ya benki au mlengwa kupewa fedha mkononi.

"Kumekuwa na changamoto kadhaa kwenye uhawilishaji fedha kwa njia ya simu,. Ili kuepukana na changamoto hizo kwa sasa, walengwa watapokea fedha hizo kwa njia ya benki au kuchukua moja kwa moja," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya TASAF kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa, Prisca Kayombo, Mratibu wa TASAF wa Mkoa, Nyasilu Ndulu, alisema Sh. bilioni 9.24 zimepokewa kwa ajili utekelezaji wa miradi hiyo.

"Hadi sasa kaisi cha Sh. bilioni6.03 sawa na asilimia 65 ya fedha zilizopoewa zimeshatumika katika ujenzi wa miradi mbalimbali kama ya afya na elimu," alisema.

Katika sekta ya afya, TASAF imewezesha kujengwa kwa zahanati tisa, Nyumba 14, majengo ya wagonjwa wa nje (OPD) mawili, jengo la upasuaji moja, jengo la kuhifadhia maiti , wodi za mama na mtoto tano na maabara moja.

"Kwa upande wa sekta ya elimu tumejenga vyumba 60 vya madarasa, ofisi 27 za walimu, matundu ya vyoo 186, maktaba moja, nyumba za walimu nne, majengo ya utawala manne, vyumba vya maabara vinane na mabweni 11," alisema.

# MAISHA

SEPTEMBA 17, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 13

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15




## KATUNIKA


Ukurasa 16



# VIDOKEZO MUHIMU Kwa mwanamke jasiri

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | 1 | 4 | 2 |
| 4 | 2 | 3 | 1 |
| 1 | 3 | 2 | 4 |
| 2 | 4 | 1 | 3 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| B | | N | G | U | R | U |
| W | | | | G | | S |
| A | | B | U | U | | H |
| W | A | O | | M | T | U |
| A | | M | B | U | | N |
| N | | B | | | | G |
| I | D | A | K | E | | I |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

NOA, FIA, WAO, KUU, UKATA, OMBWA, FUNDA, BWAWA, AOKOTWA, SHUKURU

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO Peter alikuwa akimsaidia mama yake kumwagilia maji maua katika bustani iliyopo mbele ya nyumba yao.

Wakati wakiendelea kumwagilia maji Peter alimuuliza mama yake kuhusu tabia ya nyuki kupenda maua.

Peter: Eti mama kila kwenye maua kuna nyuki?

Mama: Ndio mwanangu, ni lazima nyuki watakuwa karibu na maua?

Juma: Kwani kila ua lina nyuki wake? Mbona mwalimu alituambia kila nyuki hufuata ua lake?

Mama: Hapana huo ni msemo unaomaanisha kila zuri linatokana na chanzo chake.

**SWALI**
**Taja matumizi tofauti ya chakula aina ya karanga**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Hausigeli alininyang'anya mume nikitizama!

KARIBU tena msomaji leo tuangaze kidogo anga la mahausigeli wetu. Ni wafanyakazi muhimu lakini pia yafaa kuweka tahadhari kubwa kwani baadhi yao ni hatari, wachunguzwe kabla ya ajira.

Wako ambao ukiwaona mara ya kwanza utafarijika sana kwamba umepata lakini kumbe baada ya kipindi kifupi umepatikana. Utawaona watulivu, wanyenyekevu na lafudhi nzuri kwa maneno watamkayo midomoni kumbe ndani yake ni sumu ya mamba.

Naam. Wako baadhi ya wasomaji wa safu hii wana shuhuda nyingi kuhusu wafanyakazi hawa wa ndani. Yuko jamaa yangu mmoja alinisimulia yaliyomsibu baada ya kumkaribisha nyumbani msichana aliyeletewa bila kujua kuwa ni mke mwenzie. Ilikuwaje? Akasimulia kupitia ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani.

"Anti, hawa mahausigeli wa kuletewa ni balaa tupu. Huwezi kuamini mimi hausigeli kaninyang'anya mume hivi hivi natizama kwa macho. Hii mambo ya kuletewa achana nayo kabisa. Binti huyo aliniongopea mama yake alishakufa, hivyo mama wa kambo akawa anamnyanyasa. Eti kwao ni Singida lakini nimekuja kugundua ni Mmbulu kutoka Karatu huko Arusha. Nawashauri wenzangu wasipende kuletewa msichana bila kujua anakotoka.

Mwenzenu nimeachiwa watoto wawili na ni mume wa ndoa. Nasikia ameshazaa naye (naomba jina langu lisitajwe)".

Mpenzi msomaji, nilipomwuliza kama mumewe alisharejea kuona watoto akajibu: "Alihama kabisa na huu ni mwaka wa tano. Kuna siku alikuja kusalimia watoto lakini hakulala kwangu alifikia gesti. Hata matumizi hakuna.

Naamini mwisho wa ubaya ni aibu. Mungu yupo nimemwomba wakati wote anitetee. Nilishamuomba talaka hakunipa ananipiga kalenda tu", anamaliza ujumbe wake.

Mpenzi msomaji, bila shaka umemsikia mwenzetu huyu. Mchezo huu wa baadhi ya kinababa kuwageukia mahausigeli upo sana katika familia zetu. Kama hausigeli hakuvunja ndoa, basi anakuwa nyumba ndogo ya baba mwenye nyumba.

Baba wengine bila aibu wamewanunulia viwanja na kuwajengea au kuwanunulia nyumba kabisa. Uroho huu wa baadhi ya wanaume ni tatizo kubwa sana japo wanaokumbana na dhahama hii hugumia maumivu rohoni bila kupiga kelele.

Kinamama wengine huamua kuwa wapole wakihofia kupoteza hadhi zao za ndoa na kufikiria jinsi ya kuanza tena maisha endapo wanazihama nyumba zao za ndoa, wanashindwa na kuvumilia. Hongera sana kwao!

Kinababa wengi wanaodanganywa na penzi la wizi iwe kwa mahausigeli au kwa wanawake wa nje ya ndoa, wengi wamejikuta katika dhiki baada ya ile raha aliyoikimbilia kuchujika kama tui la nazi na kuanza tena kutamani penzi la kwanza.

Wapo waliokimbilia nje na mchecheto ulipoisha wakazitamani tena nyumba zao. Baadhi hurudi kwa aibu, wengine hufia huko huko baada ya kuvuruga kabisa boma, ikiwemo kuhamisha mali ambazo baadaye ziliyeyuka kama theluji.

Kinababa hawa wanaozipiga kisogo ndoa zao, yawezekana siyo kwa makusudi bali roho asi zinazowashambulia. Lakini wengine ni kukosa walichotarajia kutoka kwa wake zao.

Wakati wa mahusiano, wengi hawajuani kwa undani. Lakini baada ya ndoa, ndipo tabia nyingi hujifunua kati yao. Mfano baba alikuwa mnywaji kiasi lakini sasa ni mlevi wa kutupwa.

Alikuwa anamwamini mkewe akimwachia fedha za matumizi nyumbani lakini baada ya familia kuongezeka, anaanza ubahili.

Baba alizoea arudipo kazini mama kama yupo ndiye anayempokea, humpa pole na pia kumwandalia chakula, maji ya kuoga na hata chumbani. Alizoea kuandaliwa nguo za kazini na kadhalika. Lakini kazi hizi, nyingi anazifanya hausigeli.

Hapa mama ameacha jukumu lake la msingi na kuruhusu baba huyu avutwe na hisia kwamba huyu binti ndiye anayemjali kuliko yeye. Sasa akianza kumkonyeza, naye akajibu, nani alaumiwe? Hapa kuna tatizo kubwa.

Kinamama wengi wamesahau wajibu wao kwa waume zao, hivyo kutoa mwanya kwa waume kuparamia mahausigeli. Au siyo msomaji wangu?

Wengine ni hulka tu, baba anahama nyumba na kwenda kuanzisha maskani mapya. Kama ziko kasoro wanapaswa kuzijadili ili wote wajirekebishe.

Hata hivyo, kwa wale kinababa wenye viburi vya mali, pesa niwaambie kwamba kusaliti ndoa iliyokufuta vumbi kwenye kope ni dhambi kubwa. Na dhambi hii itakuandama hasa kutokana na kilio cha mkeo na watoto. Kwa usaliti huu wengi wanaishia pabaya.

***Wiki ijayo: Hausigeli anaendewa kwa mganga asiache kazi! Je, una maoni au kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kama taifa tukubali kuna mahali tumekosea

KITABU cha Ujamaa kilichondikwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere Julai, 1968, kimeelezea kuhusu azimio la kukubali aina fulani ya maisha.

Mwalimu Nyerere amesema katika hali yetu ya sasa ya uchumi na katika umasikini wetu, azimio la kukubali aina fulani ya maisha linaweza kuonekana kama jambo la vitabuni tu.

Lakini ukweli ni kwamba kuna baadhi ya vitendo ambavyo tutakataa kufanya au kuvikubali kila mtu binafsi au taifa zima, hata kama matokeo ya vitendo hivyo vingeleta ongezeko la uchumi na kutafsiri maendeleo kwa kukua.

Nikiri japo umri wangu ni mdogo, nimekipitia kitabu cha Ujamaa kwa kukisoma tena ili kujiridhisha na nia njema ya Mwalimu kulifunda taifa akiwa ameacha kitabu hicho kama wosia wake kwa Watanzania.

Ndiyo! Nimeanza na hoja za Mwalimu Nyerere baada ya serikali, kupitia kwa Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko, kukiri kwamba sera na sheria za ardhi za Tanzania ni miongoni mwa sheria bora zinazotambuliwa na nchi nyingi duniani, kwa vile zinaelekeza kuwapo ushirikishwaji wa wadau na jamii kwa ujumla katika masuala ya utawala wa ardhi.

Kwamba pamoja na ubora huo, bado maboresho ni muhimu kufanyiwa sheria hizo ili kuwa bora zaidi na kukimbia na kasi kubwa ya ukuaji wa teknolojia katika dunia ya sasa.

Sikushangaa kabisa Naibu Waziri Mkuu Biteko, kukiri hayo wakati alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika kongamano la nne la Taasisi za Ardhi Afrika lililotanguliwa na ajenda ya 'Upatikanaji wa Hakimiliki za Ardhi.'

Biteko amenukuliwa akisema: "Sisi Tanzania pamoja na ubora wa sera na sheria zetu, bado kuna sehemu tunalegalega. Na sisi tunahitaji kujifunza kwa wengine wenye uzoefu zaidi yetu na sisi tunahitaji kufundisha wengine. Naamini mtachukua hatua ya kufanya maboresho mtakayoona yanahitajika."

Maana yake ni kwamba tumefeli katika baadhi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi. Ujanja ni mwingi na urasimu bado uko ardhi.

Kumpa mwekezaji hati ya umiliki wa miaka 99 ili aje atusaidie kuzalisha kahawa kwa njia ya kisasa, halafu baada ya muda mfupi akabadili gia angani na kulima ndizi kama Wachaga, Wanyakyusa, Wahaya na Wasambaa ni kulikosea taifa letu na kukiuka makubaliano ya mkataba wa uwekezaji.

Licha ya kwamba viongozi wetu wakuu wa nchi wanafanya kazi iliyotukuka, bado tunataka mabadiliko makubwa ya sheria na sera za ardhi ili watu wetu wasiendelee kunung'unika .

Yako mambo mazuri yamefanyika na mengine yanakuja, baada ya Tania kusaini mkataba na Benki ya Dunia (WB), wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 150 kwa ajili ya kuboresha usalama wa milki za ardhi (Land Tenure Improvement Project- LTIP).

Malengo ya jumla ya mpango huu ni kutoa hati za hakimilki milioni 2.5 ifikapo mwaka 2026.

Tunataka isiwe siasa, ukiwa ni mradi wa kwanza kupata fedha nyingi katika sekta ya ardhi kutoka Benki ya Dunia Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kwamba Watanzania kila mwenye kipande cha ardhi hata kama ni kidogo, tuhakikishe anakua na hati miliki kwa faida yao na vizazi vijavyo. Changamoto nyingi za ardhi zinazowakabili Tanzania na hata Bara la Afrika, ni zile zinazotokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na upungufu wa rasilimali fedha.

Kama taifa ifike mahali tuwe na mkakati mahusussi wa waatalam wetu kujadili hizo changamoto na kuja na majibu ya namna gani tutafanikiwa katika hili. Bila ardhi hakuna maisha. Ifike mahali tukubali kama taifa kuna mahali tumekosea.

Tuwe na mpango wa kujifanyia tathimini na ufuatiliaji wa majukumu yetu ya kila siku ili kuleta matokeo chanya kwenye utendaji kazi wa serikali.

Tuyafanyie kazi maeneo yote yenye udhaifu na kuweka mikakati ya kuongeza bidii zaidi kwa yale maeneo ambayo wamefanya vizuri.

Mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa shughuli za serikali unaoandaliwa, uweke kipengele cha mrejesho kwa idara na taasisi zilizofanyiwa tahmini pamoja na kutoa mrejesho wa utekelezaji wa maelekezo ya viongozi wa juu.

Na ripoti za za tathmini na zifanyiwe kazi na idara husika ili maeneo yenye changamoto yawekewe mkakati wa muda mfupi na mrefu wa utatuzi wa changamoto hizo.


Watu wa ardhi, wafanyiwe tathmini ya utayari (Readiness Assessment) ili kubaini changamoto na fursa walizonazo ili kuondoka urasimu katika ofisi za ardhi za Wilaya, Ofisi na Makamishna Wasaidizi wa Ardhi na Msajili wa Hati.

Huko kwenye hizo ofisi, kuna mambo ya ajabu. Njoo kesho, kesho kutwa. Kupata hati ni mlolongo mrefu uliojaa viashiria vya njoo na chochote.

**Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI





Ilikuwa siku ya furaha kwa Said Haji Msokame na Zamzam Omary Juma baada ya kufunga pingu za maisha. Harusi hiyo ilifanyika Agosti 20 mwaka huu huko Mbagala Charambe na kisha sherehe ya kuwapongeza iliandaliwa huko Kimara Temboni mkoani Dar es Salaam.






# MITINDO









## TUELEWANE KWENYE SUTI

UNAFAHAMU kuwa uvaaji wa suti unakuwa na vigezo muhimu ambavyo unatakiwa kuvifuata ili kukamilisha vazi lako.

Uvaaji wa suti ni zaidi ya kuwa mtanashati na maridadi, kwani lazima kuzingatia mahali, tabia binafsi, taratibu za maisha na utunzaji.

Unaweza kujiangusha mwenyewe wakati unapovaa suti kama hujui namna ya matumizi ya vifungo hata kama umenunua kwa gharama kubwa.

Kuna aina mbalimbali za suti ambazo watu wanavaa, lakini zilizo maarufu ni zile za vifungo vitatu, viwili na kimoja.

Koti la kifungo kimoja

Suti ya aina hii inakamilika ni lazima kuvaa shati ndani la kubana. Koti la kifungo kimoja au wengi wanaita 'bleza'.

Koti la aina hii hulazimiki kufikiria kama unataka kulifunga au la.

Sharti lake kuu ni pale unaposimama unatakiwa kufunga kifungo cha koti  na unatakiwa kuweka wazi unapokaa.


Koti la vifungo viwili

Koti la vifungo viwili linapendwa kuvaliwa na idadi kubwa ya wanaume kutokana na umaridadi wake.

Hata hivyo, wengi hawafahamu kwamba unapovaa vazi hili unatakiwa wakati umesimama ufunge kifungo cha juu pekee na unapokaa vifungo vyote sharti vifunguliwe.

UREMBO

Na Mary Geofrey



# VIDOKEZO MUHIMU

## Kwa mwanamke jasiri

KILA mwanamke mwenye haiba ya kike anatamani kuwa mrembo na kuonekana mwenye mvuto kwa watu wanaomzunguka.

Urembo wa asili ni salama zaidi kwa kila mwanamke ili udumu na usichuje.

Kupitia safu hii, tutakumbushana mambo muhimu ya kuzingatia ili kuendelea kudumisha urembo wa mwanamke.



**Moisturize Daima**

Mwanamke ambaye anajua thamani ya urembo wake ana fahamu umuhimu wa kulainisha ngozi yake.

Ifanye kuwa tabia yako mpya baada ya kutoka ku oga upake moisturizer yako.

Ukitumia mafuta haya uwe na uhakika ngozi yako itakuwa laini, ya asili na yenye mvuto wakati wote bila kuchuja.

**Kulala muda wa kutosha**

Mara tu unapojua kuwa una siku au tukio kubwa linalokaribia, ratibu usingizi wa mrembo wako.

Kila binadamu anatakiwa kutumia saa 8 kila siku kwa ajili ya kupumzisha mwili wake, sasa ukilala muda pungufu kwa muda mrefu ngozi yako itachuja na kukosa mvuto.

Kulala kwa muda mrefu kunafanya ngozi inang'aa, nywele zinapata afya, kuonekana bora na kila kinachotegemea usingizi kinastawi kwenye mwili wako.

**Ng'oa nyusi zako**

Ikiwa unataka kuhakikisha kuwa unaonekana mrembo kiasili basi hakikisha unang'oa nyusi zako mara kwa mara.

Kuwa na nyusi kamili kutakufanya uso wako wote uonekane mzuri na kuondoa zile ambazo zimechoka na wakati mwingine kuingia hadi machoni

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Saladi ya viazi na 'mayonnaize'

WENGI tumezoea kula saladi ya kawaida ya kukata nyanya, kitunguu, karoti na matango.

Familia nyingi zimekuwa zikitumia saladi za aina hiyo kwa sababu ni rahisi kutengeneza na pengine hawajui namna ya kutengeneza nyingine.

Leo katika safu yetu ya mapishi tutaelezana namna ya kutengeneza saladi za aina ya viazi na mayonnaize.

**Maandalizi**

Viazi saba, maharage machanga ya kijani kikombe kimoja, karoti kikombe kimoja, mahindi kikombe kimoja, njegere kikombe kimoja na mayonnaise vijiko vitatu vya supu.

Kitunguu saumu vipande vitatu, chumvi kiasi na pilipili manga nusu kijiko cha chai.

**Namna ya kutayarisha**

Chemsha viazi kiasi visiive sana hadi kuvurugika, anza kumenya na kata vipande vidogovidogo na weka pembeni.

Menya vizuri karoti zako na uzikate vizuri vipande vidogo vidogo na uweke pembeni.

Chemsha maharage machanga, mahindi na njegere, vikianza kuiva weka karoti.

Weka maji ya kuchemshia yawe ya kiasi pembeni.

Karibu na kuiva tia karoti. Maji ya kuchemshia yawe ya kiasi kidogo tu.

**Namna ya kutengeneza**

Anza kuchuna au saga kitunguu swaumu, changanya vizuri na mayonnaise, chumvi na pilipili manga. Kisha mimina katika bakuli pamoja na mchanganyiko wa viazi na mboga, maharage, ikiwa tayari.

Saladi yako itakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa na ina yoyote ya chakula.

Unaweza kula asubuhi, mchana na jioni.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Dondoo za kusafisha dirisha la nyumba

DIRISHA ni moja ya vitu vinavyochangia kung`arisha nyumba. Lakini ili dirisha liendelee kuwa bora na kung`arisha nyumba, lazima lisafishwe.

Endapo hutaweka kipaumbele katika jambo hilo, usishangae kuona mvuto wa nyumba yako unaanza kufifia kidogo kidogo na mwisho wake ukaichukia nyumba kabisa.

Usafishaji wa dirisha ni lazima uwe na muda maalum ambao hakuna jua kali. Hiyo ni kwa sababu unaposafisha wakati wa jua kali, maji unayomiminia katika dirisha lako, hukaushwa hata kabla ya kupitisha sponji, hivyo itakuchukulia muda mwingi na pia haliwezi kung`aa vizuri na huacha ukungu.

Wakati unasafisha unatakiwa uwe pia na dawa maalum au kama unatumia maji si vibaya ukadondoshea kidogo vitone hata viwili vya maji maalumu yenye mchanganyiko wa limao, maarufu kama 'vinegar'.

Baada ya hapo unalowanisha sponji yako au kitambaa laini kwa kuchovya kwenye maji hayo na kuanza kusafisha katika dirisha lako.

Hakikisha unasafisha kuanzia juu kushuka chini, ili uchafu wote utiririkie huko kwa sababu kufanya hivyo kutakuhakikishia kuwa hakuna uchafu utakaodondokea kwenye sehemu ambayo umeshasafisha tayari.

Kama eneo la dirisha unalotaka kusafisha ni chafu sana au kuna vumbi jingi au utando wa buibui, futa kwanza kwa kitambaa kikavu kabla ya kusafisha na maji.



Uwe makini kuchunguza uchafu ulioko kwenye kona za madirisha yako.

Epuka sana kuweka maji mengi kwenye sponji au kitambaa unachotumia kusafishia ili yasimiminikie chini sehemu ambayo si ya dirisha iwe ukutani au sehemu nyingine isiyohusika.

Hakikisha unasuuza na kukausha dirisha lako kwa kutumia kitambaa kikavu na laini na baada ya hapo rudia tena kwa ajili ya kuling`arisha.

Kama utakuwa na dawa maalum ya kusafishia, itapendeza zaidi kuipulizia kidogo katika dirisha lako huku ukifuta kwa kutumia kitambaa cha pamba ambacho hakitoi nyuzi.

Hakikisha dawa unayotumia kusafishia ni ile ambayo haiwezi kuharibu ama kupausha mbao za dirisha lako.

Kama dirisha lako ni la kioo, hakikisha sponji au kitaamba ulichotumia kusafishia kioo ni tofauti na kile unachosafishia kwenye fremu au kona za dirisha lako.

Katika maeneo ya fremu na kona, safisha kwa kutumia kitambaa kigumu zaidi ambacho kitabeba uchafu wote kwa sababu eneo hilo

## Maajabu matano mapambo

Na Restuta James

WATAALAMU wa mapambo ya ndani wametoa orodha ya mwenendo wa mapambo ya ndani katika kipindi cha miezi sita iliyopita.

Wameeleza kuwa matumizi ya mbao, rangi tulivu, kuchanganya mwonekano wa kisasa na wa zamani na bustani ni maeneo yanayoendelea kustawi zaidi.

Mtaalamu wa mapambo, Ndigwako Mwakyelu, anasema rangi ya bluu na kijani tulivu, ndizo zinazopendelewa zaidi huku nyeupe na nyeusi, zikitajwa kama rangi muhimu za kuongeza nakshi ndani ya nyumba.


Anasema mchanganyiko wa mapambo ya zamani na sasa hasa samani, ni eneo linaloongeza mwonekano wa kipekee ndani ya nyumba na bustanini pia.

"Unaweza kuweka meza ya kula yenye mwonekano wa kizamani lakini picha za ukutani na meza ya bufee ikawa ya kisasa, huu ni mchanganyiko mzuri sana wa kupendezesha nyumba," anasema.

Ndigwako anasema mabadiliko ya tabianchi yamegusa kipekee eneo la mapambo, hivyo hamasa imekuwa kutumia vitu vinavyotunza mazingira, kuanzia aina ya maua ya kupanda msisitizo ukiwa ni yale yanayosafisha zaidi hewa.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
HAIPENDEZI MKE KUWA MBEA KWA MUMEWE...NANI KAKWAMBIA NAOA LEO USIKU?
UMEROPOKA MWENYEWE USINGIZINI UNAMUOA BINAMU!
UNANIHA-MISHA SHULE SABABU YA VIBOKO?
INAONYESHA UNA NYOTA YA 'NGOMA' KUPIGWA BILA KUHISI MAUMIVU!
NIAHIDI KAMA NIKISEMA KUWA 'NIMEBAKA' ITABAKI SIRI
NAJIAPIZA HAKYA-MUNG' HATA NIWE MWENDAWAZIMU SISEMI NG'O!
NIKISEMA NIFE HAPA HAPA NIOZE
NNA NYUMBA NDOGO LAKINI MWANAO HATOJUA KABISA!
KWELI KABISA HATOJUA KWA HAPA ULIPOROPOKA!
NYIE WAZAZI WENGINE MKIFIKA KWA WALIMU UNAPIGA MWANAO KAMA UNAUA NYOKA!
WEWE ACHA KUROPOKA!
ANAONGEA UKWELI MKIFIKA KWA WALIMU MNA-ADHIBU KWA USONGO
ETI LENGO AONEKANE MZAZI MKALI KUMBE...!
TENA USI-OMBE MZAZI AWE KALIPU-LIZA!
MKUKI MTAMU KWA NGURUWE!
BABUWEEE! UNANITIBU AU UNANIKOMESHA? UGANGA GANI KUTWA NZIMA UNAIMBA?
UNA BAHATI NIMEPANDISHA 'JINI SEBENE' KULA SONGI
TIVII GANI UNAMUONA MTU MREFU KANYOOKA KAMA KAMEZA MNAZI!
DAMPO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...FUNUA KOMBE MWANAHARAMU AUMBUKE...

# Ufaransa yadai balozi wake anaishi kama mateka Niger

**NIAMEY,** NIGER

RAIS wa Ufaransa Emmanuel Macron, amesema balozi wake nchini Niger na wafanyakazi wengine wanaishi kama mateka ndani ya jengo la ubalozi uliokoa katika mji wa Niamey.

Kiongozi huyo aliwashutumu watawala wa kijeshi kwa kuzuia kupelekwa chakula ndani ya ubalozi huo.

Rais Macron alieleza kwamba ofisa huyo hawezi kutoka nje baada ya kuondolewa kinga ya kidiplomasia na amekataliwa kupewa chakula.

Maandamano ya kutaka wanajeshi wa Ufaransa waondoke yalifanyika nchini humo na viongozi wa kijeshi walitoa saa 48 kwa balozi wa Ufaransa nchini humo Sylvain Itte kuondoka mara moja.

Uamuzi wa kumtimua balozi huyo ulichukuliwa bada ya kupinduliwa kwa serikali ya Rais Mohamed Bazoum Julai 26.

Hata hivyo, balozi huyo hakuondoka ndani ya muda huo uliotolewa huku serikali ya Ufaransa ikigoma kutambua utawala wa kijeshi.

Ufaransa inao wanajeshi wapatao 1,500 nchini humo na ilisema mapema mwezi huu kwamba kupelekwa tena kwa wanajeshi kunaweza kujadiliwa na Bazoum pekee.

**DW**



Magari yakiwa yamesombwa na mafuriko na kurundikana kwenye mtaa mmoja wa mji wa Derna nchini Libya. Pichani ni waokoaji wakiendelea na kazi ya utafutaji wa miili ya watu waliofariki dunia kutokana na mafuriko hayo. Hadi jana, zaidi ya miili 10,000 ilipatikana. **PICHA: REUTERS**

# Nchi tatu zapinga azimio la Ulaya

**WARSOW,** POLAND

NCHI za Poland, Slovakia na Hungary zimetangaza kuendelea kuweka vizuizi vyao katika uagizaji wa nafaka kutoka Ukraine.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya Tume ya Umoja wa Ulaya kutangaza kwamba haitopanua marufuku inayoathiri nchi tano.

Marufuku hiyo iliyokuwa imetangazwa na Umoja wa Ulaya mwezi Mei iliziruhusu Poland, Bulgaria, Hungary, Romania na Slovakia kuzuia mauzo ya ndani ya ngano, mahindi na mbegu za alizeti kutoka Ukraine.

Lakini nchi hizo ziliruhusu usafirishaji wa bidhaa hizo kuuzwa nje ya nchi zao.

Kamishna wa Biashara ndani ya Umoja wa Ulaya Valdis Dombrovskis alizitaka nchi hizo kujiepusha na hatua za upande mmoja dhidi ya marufuku ya uagizaji wa nafaka za Ukraine.

**DW**

# Wakenya walalamikia kupanda mafuta

**NAIROBI,** KENYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Petroli nchini Kenya, imetangaza kupanda kwa bei za mafuta na kufikia rekodi ya juu na kuibua malalamiko kwa wananchi wa taifa hilo.

Kulingana na tangazo la mamlaka hiyo, bei ya reja reja ya lita moja ya mafuta ya petroli imezidi shilingi 200 za Kenya sawa na dola 1.36 za Kimarekani, bei ambazo hazijawahi kushuhudiwa.

Chini ya bei hizo ambazo zimeanza kutumika tangu Ijumaa na zitadumu hadi Oktoba 14, lita moja ya petroli katika mji mkuu wa Nairobi imepanda kwa takriban shilingi 17 na itauzwa kwa shilingi 211.64 na dizeli ni shilingi 200.99.

Raia wanalalamika kuongezwa mzigo wa gharama za juu za maisha kutokana na kupanda bei kwa bidhaa nyingi muhimu, msururu wa kodi mpya na kuporomoka kwa thamani ya shilingi.

Ripoti za vyombo vya habari vya Kenya zilisema kuwa nauli za matatu yani mabasi madogo yanayotumiwa na Wakenya walio wengi, pia zinatarajiwa kupandishwa huku Chama cha Wamiliki wa Matatu kikitangaza ongezeko la asilimia 20 la nauli nchini kote.

Mawaziri wa serikali wamelaumu kwa kiasi fulani kupunguzwa kwa uzalishaji wa mafuta kulikotangazwa mapema mwezi huu na wazalishaji wakuu Saudi Arabia na Russia kumesababisha bei ya mafuta ghafi duniani kupanda.

Waziri wa nishati wa Kenya Davis Chirchir aliieleza kamati ya nishati ya bunge kwamba hakuna chochote tunachoweza kufanya kupunguza bei ya nishati hiyo.

Waziri wa Biashara na Viwanda Moses Kuria, alionya kupitia mtandao wa X, kwamba Wakenya watarajie bei ya mafuta kupanda kwa shilingi 10 kila mwezi hadi Februari.

Ripoti za vyombo vya habari zilisema serikali inataka kuongeza kodi zaidi ikiwa ni pamoja na kuongeza VAT na ushuru unaolenga wakulima na wamiliki wa magari kulingana na mkakati wa mapitio wa wizara ya fedha wa mwaka 2026/27.

Wakenya wengi wamemshutumu Rais Ruto kwa kuvunja ahadi alizotoa kwenye kampeni za uchaguzi wa mwaka jana, alipoahidi kuboresha maisha ya watu wa kawaida.

**DW**

# Wanasheria wataka Trump azibwe mdomo

**WASHINGTON,** MAREKANI

MWENDESHA mashtaka anayeongoza kesi ya kuingilia uchaguzi dhidi ya rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump amemtaka jaji kuweka amri ya kukataza mawakili, wahusika, au mashahidi kuzungumzia juu ya mashtaka hayo kwa umma.

Wakili Maalum Jack Smith, alisema kwamba amri hiyo itazuia unyanyasaji wa mashahidi.

Baada ya kutolewa ombi hilo, Trump alijibu mtandaoni, akishutumu timu ya Smith kwa utovu wa nidhamu.

Trump amekana kuhusika na kula njama ya kutengua uchaguzi wa mwaka 2020.

Ombi hilo lilifunguliwa na Jaji wa Mahakama ya Wilaya Tanya Chutkan na kuwasilishwa wiki moja kabla na ni miongoni mwa hati nyingi za mahakama kutoka kwa kesi hiyo ambazo zilitolewa Ijumaa.

Waendesha mashitaka walisema agizo lao lilipendekezwa - ambalo hawataliruдia tena kama amri ya zuio iliyobainishwa ambayo ni muhimu kwenye kuzuia taarifa potofu, vitisho na kuathiri mwenendo wa kesi hiyo.

Iwapo amri hiyo itaidhinishwa, itapiga marufuku Trump kutoa matamshi kuhusu utambulisho, ushuhuda, au uaminifu wa mashahidi watarajiwa na maelezo kuhusu upande wowote, shahidi, wakili, wafanyakazi wa mahakama, au majaji watarajiwa ambayo ni ya kudhalilisha, uchochezi, au kutisha.

Haimuwekei vizuizi vyovyote kwa Trump kunukuu kutoka kwenye hati za rekodi za umma au kutangaza kuwa hana hatia.

Vizuizi vyovyote vilivyowekwa katika marekebisho ya kwanza ya rais huyo wa zamani juu ya uhuru wa kujieleza, haswa anapowania urais mwaka wa 2024, vitaanzisha pingamizi la kikatiba mahakamani.

Wiki iliyopita, mawakili wa Trump walimwandikia Jaji Chutkan, wakisema kuwa ana upendeleo na kumtaka ajiondoe kusikiliza kesi hiyo.

**BBC**

MAKALA

# HONGERA JKT, HONGERA VIJANA WETU



Na Magabilo Masambu

MKUU wa wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda, amehitimisha rasmi mafunzo ya kozi ya vijana kwa mujibu wa Sheria kundi la lazima operesheni miaka 60 ya Jeshi la Kujenga Taifa, sherehe ambazo zimefanyika katika uwanja wa Meja Jenerali Samwel Kitundu 833 Kikosi cha Jeshi Oljoro, Arusha.

Mkuu huyo wa wilaya pamoja na kuwapongeza wakufunzi wa mafunzo hayo kwa kazi kubwa waliyofanya, amewaasa wahitimu kwenda kuyatumia kwa vitendo lakini pia kujiepusha na matumizi yasiyo sahihi ya mitandao ya kijamii.

"Ninyi vijana mnaomaliza mafunzo, nendeni mkalitumikie taifa muwapo vyuoni au sehemu nyingine kwa moyo mmoja na kwa uzalendo mkubwa, Taifa letu linawategemea sana kuwa viongozi wa siku zijazo. Kaonyesheni kwa vitendo yale yote mliyojifunza ili kutimiza malengo ya mafunzo na kujitofautisha na wale ambao hawajapata mafunzo haya.

Pili, epukeni matumizi yasiyo sahihi ya mitandao ya kijamii, ili msije mkashindwa kufikia malengo yenu kwa kutenda makosa ya kimtandao yatakayopelekea kushitakiwa na hata kufungwa," anasisitiza Kaganda.

Brigedia Jenerali Abubakari Charo, Mkurugenzi wa Polisi Jeshi, kwa niaba ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, ameeleza juu ya miongozo ambayo hutolewa mara kwa mara ili kuendelea kuyaboresha mafunzo ya vijana.

Anasema kwa kutambua umuhimu wa vijana katika taifa la Tanzania, jeshi hutoa miongozo mbalimbali ya jinsi ya kuboresha mafunzo ya vijana ili yaendane na madhumuni ya kuanzishwa kwake. Anasema mafunzo ya awali ya JKT yanamjenga kijana kuwa tayari kujifunza mafunzo mengine ya stadi za maisha na stadi za kazi. Kwa hiyo kijana atakuwa na nidhamu, ukakamavu, uzalendo, uhodari, uvumilivu, kujiamini na moyo wa kupenda kufanya kazi.

Mwakilishi wa Mkuu wa JKT, Kanali Robert Kessy, akatumia nafasi hiyo kuwashukuru wazazi na walezi waliowaruhusu watoto wao kujiunga na mafunzo hayo huku akisema kwa namna ya kipekee, shukrani nyingi ziwaendee wazazi na walezi wa vijana waliohitimu, kwa moyo wao wa kuwaruhusu kuhudhuria mafunzo haya.

Sambamba na shukrani hizo, aliwaasa wahitimu kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa amani, ulevi, utumiaji wa dawa za kulevya, ulaji wa vyakula au utumiaji wa vinywaji vyenye kuhatarisha afya.

Kamanda wa 833KJ, Luteni Kanali Victor Faustine akaeleza jinsi mafunzo yalivyokuwa. Mafunzo haya yamechukua muda wa majuma 12 na vijana wamejifunza masomo ya darasani (nadharia), uwanja wa medani, kazi za mikono na uzalishaji mali lengo likiwa kukuza moyo wa kizalendo, kuwajengea ujasiri, uwezo wa kutumia muda vizuri na kuwafanya wajitambue kuwa pia ni sehemu ya jamii ya Watanzania wanaopaswa kupata mafunzo ya JKT.

JKT ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 16 (National Service Act, 1964) iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002 kifungu 3(1). Sheria hii ilipitishwa ili kuwataka vijana kujitolea kwa hiari kujiunga na jeshi hilo. Kurejeshwa kwa mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria ilikuwa moja ya mambo yaliyopewa kipaumbele cha juu katika awamu ya nne ya serikali ya Tanzania chini ya Amiri Jeshi Mkuu na Rais Dk. Jakaya Kikwete.

Jeshi hilo limefanya kazi kubwa na nzuri ya kujenga moyo wa utaifa na uzalendo miongoni mwa vijana waliopitia katika jeshi hilo. Hapa ni mahali vijana wa itikadi zote, rangi zote, makabila yote, dini zote, hukutana, huishi pamoja na kufanya mafunzo na kazi kama ndugu wa familia moja.

Naweza kusema hakuna chombo chochote cha malezi ya vijana kinachoizidi JKT katika kazi hiyo, pengine hata ile tabia ya Watanzania wengi kutoulizana makabila yao inatokana na uwapo wa JKT. Vijana wazalendo wa Tanzania wanaopitia JKT huwa wanakutana na vijana mbalimbali kutoka kila kona ya nchi, ndiyo maana hawana muda hata wa kuulizana makabila kwa vile wote hujiona ni wamoja.

Katika kufunga mafunzo, hamasa waliyoionyesha vijana ikanifanya nitamani kurudi shuleni ili niwe miongoni mwao. Mambo waliyoonyesha utadhani wamejifunza miaka mitatu. Ukakamavu wao, nidhamu na michezo mbalimbali waliyoionyesha hakika JKT mmetisha sana. Hongereni wakufunzi, hongereni vijana na hongera Tanzania.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania.**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kisa cha mume aliyemtongoza mtalaka akidhani ni demu mpya*



Na Adam Fungamwango

DUNIA haijawahi kuishiwa mikasa hasa kwenye masuala ya uhusiano.

Unaweza ukadhani kwamba ni hadithi za kufikirika, kumbe ni kweli kabisa inatokea.

Kuna mtu ameshawahi kusema kuwa hakuna mwanamke mbaya duniani, kinachowatofautisha ni matumizi ya urembo, vipodozi, na matunzo.

Hili linatiwa nguvu wa visa vingi vya baadhi ya wanaume kwenda kuoa vijijini wake wanaoonekana kuwa ni wa kawaida sana.

Wanapoishi kwenye miji mikuu na kupata matunzo wanabadilika na kuvutia wanaume ambao hawana jicho la tatu. Ni kweli kabisa, kuna wanaume wao kazi yao kuchukua wanawake ambao wameshatunzwa na wenzao, wakapendeza.

Wao hawana muda ya kumchukua mwanamke kutoka mbali kijijini ambako mara nyingi wanakuwa hawana urembo na vipodozi, wao wanasubiri apendeze tu. Wako pia wanaume kwenye jicho la tatu, wanaoweza kwenda popote pale hata vijiji vya mbali wakakutana na akinadada wakiwa kwenye hali yao ya asili bila vikorombwezo na wakatambua uzuri uliojificha wakaamua kuwachukua.

Na kweli wanapofika mjini na kupata mahitaji muhimu na matunzo, uzuri wao unajionyesha bayana hata kwa mtu asiyeona.

Hili ni fundisho kwa wanaume kuwa mwanamke ni matunzo tu na si kitu kingine chochote.

Kuna wanaume wanaacha wake zao na kukimbizana na wanawake wengine barabarani wakidhani kuwa ni warembo zaidi lakini kumbe si kweli.

Ni kwamba tu wamepunguza kuwahudumia na kuwatunza wake zao, pesa zote zinaishia nje kwa mabibi wengine.

Kinamama wa Pwani wana msemo hao kwa wanaume wenye kupenda sana kutoka nje ya ndoa kwamba "Utamaliza bucha nyama ni ile ile." Maana yake ni kwamba umatamaliza wanawake wote wa dunia, lakini ni wale wale tu, hawatofautiani.

Yaani mke aliyeachwa nyumbani na hajaachiwa pesa ya kula, hana tofauti na yule wa nje ambaye anamaliza pesa zote za mwanamume.

Kilichokosekana hapo ni kwamba wa nyumbani kwa sasa hana matunzo tu.

Ukitaka kuthibitisha hili hebu nikupe kisa kimoja ambacho kimechukuliwa na kutungiwa wimbo katika bendi ya Maquis Original.

Wimbo huo ukapewa jina la 'Kaiba.' Kaiba ni mwanamke ambaye awali alikuwa ameolewa. Lakini miaka kadhaa ya ndoa, ikageuka kuwa ndoa ndoana. Akaanza kunyanyaswa, kupigwa na kukosa matunzo.

Hali ilipozidi jamaa akamtimua mwanamke na kutoa talaka haraka kwa sababu alikuwa ameshanogewa na wanawake wa nje, akimuona mkewe amekwisha na hana maana sana.

Miaka michache baadaye jamaa alikutana na mwanamke mmoja mzuri na mrembo sana barabarani.

Kwa sababu alikuwa hajaacha tabia yake akamsogelea na kuusifia uzuri wake, huku akimtongoza. Mwanamama akamuangalia, akatabasamu. Halafu akamjibu maneno mazito.

"Unachoshangaa sasa ni nini we babu, au unafikiri siyo mimi unitamani tena ehe, basi ni yule yule Kaiba,uliyokuwa unanitelekeza, unanifukuza kwa kashfa nyingi mvua ikininyeshea bila huruma eee, mama mama."

Kumbe bwana aliyekuwa akimtongoza ni mkewe wa zamani. Siku zimekuwa nyingi, amemsahau akamtongoza tena mtalaka wake.

"Usinione hivi babu nimependeza, hii ni kazi ya mwenzio babu kanithamini eee, basi mimi ni yule yule Kaiba, uliyokuwa unanitelekeza, unanifukuza kwa kashfa nyingi mvua ikininyeshea bila huruma eee, mama mama."

Kumbe jamaa alimtongoza tena kwa sababu alikuwa amebadilika, amenawiri, amependeza na hicho ndicho kilichomfanya ampende tena.

Hapa ndipo tunathibitisha kile tulichokisema mwanzo kuwa siku zote mwanamke ni matunzo.

Yeye alimtimua nyumbani huku akinyeshewa na mvua, amekwenda huko amepata mwanaume mwingine ambaye anamthamini, kumtunza na kumliwaza, mama karidhika amenawiri kuliko alivyokuwa naye, mate yanamdondoka.

"Hata hivyo, mama ngoya ee, kwa kweli dunia kabla hujafa hujaumbika eee, namshukuru Mungu umeniacha salama eee, mama ngoya eee, mi' Kaiba nimetulia, mama ngoya eee, ngoya, mi' Kaiba ee."

Kaiba msimamo wake upo pale pale, inaonekana bado mateso yale hajamuondoka kichwani na imekuwa ni moja kati ya kumbukumbu mbaya katika maisha yake.

Anamwambia mtalaka wake kuwa anamshukuru Mungu kwa kumuacha salama, maana angeweza kumuacha akiwa na makovu au ulemavu, ameachwa akiwa hai na afya njema na sasa amepata mwanaume mwingine ametulia.

Majibu haya yanaonyesha kabisa kuwa mtalaka ya Kaiba sijui kama alimuaga mwenzake, badala yake aliondoka kwa aibu.

Unamtesa na kumyanyasa mke, unamtimua halafu baada ya miaka michache unamsahau kwa sababu amebadilika na kupendeza, unamtongoza tena, anakukumbusha na kukuumbua, ni lazima uondoke bila kuaga.

Wimbo huu ulitungwa mwanzoni mwa miaka ya 1990 na Tshimanga Kalala Asossa, wakati huo bendi ikitumia mtindo wa 'Sendema.'

Funzo kwa wanaume waliooa hapa ni kwamba wawapende, kuwajali na kuwatunza wake zao, badala ya kupaparika nje.

Namalizia tena kwa misemo ya 'hakuna mwanamke mbaya duniani', na ule wa 'utamaliza mabucha yote, nyama ni ile ile."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Kafie kwenu-11

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

CATTY alishusha pumzi ndefu. Halafu akajibu kwa sauti ndogo ya huzuni, "Usijali James, kama unajiona unaweza kuendelea na maisha yako ya kawaida sawa, ila hapa tayari umeshakuwa kwako, ukizungukazunguka uje kutuona na kutusalimia dada zako, hata sisi binadamu tunaweza tukawa na matatizo, tukaumwa, tukahitaji hata mtu wa kuja kumtuma soda tu dukani."

"Hakuna shida dada, nitaendelea na maisha yangu kama kawaida, lakini mara kwa mara nitakuwa nakuja kuwasalimia. Ila nikimkuta Carry wewe haupo sasa halafu wewe haupo sijui itakuwaje?" Akasema na kuanza kucheka.

Catty akatabasamu na kumuuliza. "Vipi, umesahau? Si ndiyo itakuwa vizuri ili uendelee kumbembeleza?

Wote wawili waliangua kicheko.

Catty alianza kuona kama ushauri wake unaanza kumuingia kijana. James naye pia ilionekana alianza kuchoshwa na dharau na kejeli za Carry.

"Usihangaike na mtu asiyekupenda siku zote. Tafuta wa saizi yako. Usipende kudhalilishwa na kila mwanamke unayekutana naye barabarani." Akakumbuka maneno aliyoambiwa huko nyuma na Catty.

***********************************

Mwezi mmoja ulipita. Taratibu ilianza minong'ono ya kutoonekana kwa James. "Yuko wapi wakati si kawaida yake?" Wengi walijiuliza.

Hakuwa mtu wa kujifichaficha, au kutoonekana bila sababu yoyote. Kwa sababu kazi yake iliyompa kipato ilikuwa ni kufanya kazi mbalimbali ndogondogo kwenye majumba ya watu.

Awali ilionekana labda yuko sehemu fulani kesho ataonekana. Lakini kadri muda ulivyozidi kwenda hakuonekana mitaa ya Kinondoni Moscow ambako amezoeleka sana kuonekana.

Iliwashtua wengi, lakini hawakuwa na la kufanya. Hakuna aliyemfahamu ndugu yake yoyote zaidi yake mwenyewe na kijumba chake kilichopo bondeni.

Kama ilivyo penye wengi pana mengi. Kila mmoja alianza kuongea lake.

Kwenye kijiwe cha kina mama Sauda, wale waliokuwa wanamsema alipokataliwa na Carry jambo hili halikuwapita.

Siku hiyo walikusanyika kama kawaida yao, wengine wakisukana nywele, wengine wakifumuana, wapo waliokuwa wanafuma vitambaa, na wapo waliofika tu kwa ajili ya soga.




**"Mmmh! Ya kweli hayo mama Sauda, au unamtetea kwa kuwa mkweo, mi si nasikia kataka kumbaka mwanafunzi huko Buguruni alikokwenda kwenye vibarua vyake, wamemdaka wakampeleka kituoni, nasikia yupo rumande." Mai naye akatoa ya kwake.**

Kama kawaida yao hukusanyika kuanzia saa 8:00 mchana wakati tayari wameshapata chakula cha mchana.

"We mama Sauda, mkweo haonekani, vipi yuko wapi, au umesikia alipokwenda?" Akauliza dada mmoja aliyejulikana kwa jina la Maimuna, lakini wenyewe mtaani wanamkatisha na kumuita Da' Mai.

"Mwenzangu we, hata najua ila kuna mmbea mmoja simtaji jina kaniambia sijui alifanya kazi wapi huko, nyumba ikapiga shoti ya umeme wakasema yeye ndiyo kasababisha wakampeleka polisi, hivi sasa yupo gerezani."

"Mmmh! Ya kweli hayo mama Sauda, au unamtetea kwa kuwa mkweo, mi si nasikia kataka kumbaka mwanafunzi huko Buguruni alikokwenda kwenye vibarua vyake, wamemdaka wakampeleka kituoni, nasikia yupo rumande." Mai naye akatoa ya kwake.

"Yote wanawezekana, lakini ukweli halisi bado haijajulikana."

Wakati huo Sauda naye alikuwa anatoka shule. Huyu mwanafunzi wa kidato cha pili huwa mara kwa mara anamtetea sana James pale anapotetwa na mama yake akishirikiana na shoga zake.

Humtetea kwa sababu mara kwa mara amekuwa akiwasaidia yeye na wanafunzi wenzake kwa mambo mbalimbali wanapokutana naye njiani.

Ndiyo maana wanamtania Sauda kumwambia ni mchumba wake, na mama yake wanamwita ni mkwewe.

"We Sauda nasikia mchumba wako kakamatwa huko!" Mai akamwambia muda mfupi tu baada kusimama na kuwasalimia.

"Kafanya nini?" Akauliza uso wake ukionekana kuhamanika.

"Sijui kabaka mwanafunzi huko, yupo rumande saa hizi..."

"Mmmh uongo."

"Sasa wewe ulikuwepo?"

"Na wewe ulikuwepo wakati anabaka?"

"We usinijibu hivyo, mi' siyo mtoto mwenzio."

Sauda hakujibu. Aliondoka taratibu huku akilia.

"We tutolee uchuro wako hapa, unalia nini? Kafa shangazi yako?" Mama Sauda alimfokea binti yake ambaye sasa alikuwa anaishia kwa kuingia ndani.

Alilia kwa mambo matatu, kwanza habari ya James ilimchanganya, pili majibu ya mmoja wa shoga wa mama yake.

Kingine kilichomliza ni kwa nini watu wanaonekana hawampendi James? Wanasema vibaya wakati yeye na baadhi ya wanafunzi wenzake hasa wa kike wanamuona kama ni mtetezi wao.

Huwavusha barabara anapowaona. Huwanunulia 'ice cream', na kuwatetea pindi wanapoonewa na vijana wakorofi mtaani.

Huwatisha kuwa atakayewaonea dada zake basi atakula nao sahani moja.

Na tayari alishawaambia yoyote atayewasumbua au kuwapiga waende kumueleza na atashughulika nao.

Pamoja na kwamba ana hali duni, lakini hakuna binadamu mbaya, au anayedharaulika kwa watu wote.

Mwingine ambaye hakuwa kwenye hali ya kawaida ni Catty.

Kama wengine alisikia hadithi tofauti ambazo hazijathibitishwa.

Kuna wakati pia ilikuja taarifa kuwa kuna mtu aligongwa na gari na maiti yake ilipelekwa kwenye chumba cha maiti katika Hospitali ya Taifa, Muhimbili.

"Haiwezekani! Ni lazina tufutilie tuone nini tunafanya. Kijana wa watu hana baya.

Ameishi na watu vizuri, haiwezekani tumuache tu.

Hata kama amekufa, basi tuipate maiti yake tutachangishana na majirani ili tumzike jirani yetu kwa sababu inaonekana hana ndugu. Yaani haipendezi basi kakaa na watu vizuri maiti yake izikwe na 'site.'

Catty alianza kuhamasisha jambo hilo kwa majirani na watu wengine ambao aliowaona walikuwa na urafiki wa James.

Hata hivyo muitikio ulikuwa mdogo sana. Kila mtu alikwepa. Kila mmoja alikuwa bize. Catty ni mueleewa, alijua sababu. James alikuwa ni fukara, asiyekuwa na ndugu.

Alipata upinzani hata kwa dada yake ambaye alimshangaa na kumuona mtu asiye na kazi ya kufanya.

Katika juhudi zake zote alipata watu wazima watano tu na yeye mwenyewe wa sita. Wanne alikuwa wanawaume, wanawake wawili yeye na mwenzake mmoja.

Wanafunzi 10, saba wa kike, akiwemo Saida na watatu wa kiume walijitokeza, lakini kwa sababu walikuwa wadogo hawakuruhusiwa kuifanya kazi hiyo.

Kazi ilianza kwanza ya kwenda kwenye kijumba chake ili kuangalia kama kuna nyaraka zozote ambazo ameacha.

Walipoona hakuna chochote cha kuwasaidia sasa ikaanza kazi ya kumsaka kwenye vituo vya polisi, na Hospitali zote za Dar ikiwemo kwenye vyumba vya maiti walau kupata hata mwili wake wauzike kwa heshima zote kama jirani yao.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# KETE YA MWISHO

KAMA atafanikiwa jaribio lake, basi atakuwa na bahati ya kipekee kuona msanii mkongwe akirudi katika chati ya muziki wa Marekani.

Jaribio hilo linafanywa na rapa mkongwe na tajiri wa Marekani Diddy, ambaye ametangaza kurudi studio kwa ajili ya kupika albamu yake mpya.

"Niliondoka kwa muda kidogo, nikapitia mambo mengi maishani, kisha nikapata wito huo siku moja kutoka kwa Mungu. Aliniambia wakati umefika,'" amesema Diddy mshindi mara tatu wa tuzo za Grammy.

Amesema sauti hiyo nyororo aliposikia papo hapo ilimchochea kuelekeza fikira zake tena kwenye kutengeneza muziki wake mwenyewe.

Diddy ameachia albamu yake mpya iitwayo "The Love Album - Off the Grid," jana na imewashirikisha karibu wasanii 30.

Baadhi ya wasanii waliohusishwa ni Mary J. Blige, Justin Bieber, The Weekend, H.E.R. Babyface, John Legend, Busta Rhymes, Summer Walker, Teyana Taylor, Coco Jones na Jazmine Sullivan.

"Nilikuwa kama nataka kutengeneza R&B nilikuwa nikijiuliza swali: Ikiwa ungelazimika kufanya jambo moja kwa maisha yako yote, ungefanya nini? Na hiyo ingekuwa kufanya muziki," asema.



# CHOZI LA IBRAAH FARAJA YENU

KILIO cha mwanamuziki Ibrah kutoka lebo ya Konde Gang, kinachoeleza maisha yake kuwa magumu ni kiashiria tosha kwamba sanaa muziki si sehemu ya mchezo.

Ibraah hivi karibuni alibainisha kwamba kwamba maisha yake ya Sanaa kwa sasa yako katika wakati mgumu na kwamba si rahisi kuyazoea.

Awali bosi wake Harmonize alisema kwamba kimya cha mwanamuziki huyo kinatokana na utata wa malipo kutoka kampuni ya kusambaza kazi za wasanii, Zikki Media, na kwamba wakati wowote mambo yatakuwa sawa.

Ibraah aliwataka mashabiki kumpa kumbatio la nguvu kwa wimbo wake mpya na anaweza kupata faraja kwa kukaa kimya kwa miezi kadhaa.

## ZISIKUPITE

### SANCHO KUONDOKA UNITED
JADON Sancho yuko tayari kuondoka Manchester United katika dirisha la usajili la Januari ikiwa winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 23, atasalia kuwa katika klabu hiyo hadi mwaka mpya. (***Manchester Evening News***)

### EKITIKE NJIA MOJA
KLABU ya West Ham haijafikia makubaliano ya kumnunua, Hugo Ekitike wakati wa usajili wa majira ya joto, lakini mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 21 anatazamiwa kuondoka Paris St-Germain ifikapo Januari. (***Football Insider***)

### BAYERN NA CHALOBAH
KLABU ya Bayern Munich inaweza kurejelea tena suala la uhamisho wa mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24 katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Football Insider***)

### BARCO NEEMA YAMFUATA
BOCA Juniors inajiandaa kumpa mkataba mpya, Valentin Barco anayelengwa na Manchester City ambako kutamfanya beki huyo wa kushoto wa Argentina mwenye umri wa miaka 19 kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika klabu hiyo. (***Diario AS***)

### YAMAL ALITAKIWA CITY
KLABU ya Manchester City walijaribu kumsajili, Lamine Yamal msimu huu wa joto, kabla ya winga huyo mwenye umri wa miaka 16 kusajiliwa na Barcelona ya Hispania msimu huu. (***Marca***)

### TADIBO ALIIKATAA UNITED
MLINZI wa Nice ya Ufaransa, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 23, amesema hakutaka kujiunga na Manchester United msimu wa joto kwa sababu 'hakutaka kufanya makosa'. (***L'Equipe***)

### EVERTON MAMBO MAGUMU
MKURUGENZI wa Soka wa Everton, Kevin Thelwell aliwasilisha mipango mitatu tofauti ya kusajili wachezaji kwa wamiliki wao wapya, lakini jibu lilikuwa la kuvunja moyo na kuzua wasiwasi miongoni mwa wakuu wa klabu hiyo kuhusu nia yao katika uwekezaji wa timu. (***Football Insider***)

### HINCAPIE BADO YUPO
KLABU ya Liverpool haiko karibu na mpango wowote wa kumnunua beki wa kati wa Bayer Leverkusen, Piero Hincapie mwenye umri wa miaka 21, licha ya ripoti kusema vinginevyo. (***FootballTransfers***)

### ODEGAARD, ARSENAL SAFI
KLABU ya Arsenal ina uhakika wa kukubaliana kuongeza mkataba na kiungo wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 24. (***ESPN***)

### WHITE KUZEEKEA ARSENAL
ARSENAL pia wanataka kuongeza mkataba wa beki wa England, Ben White licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 bado ana miaka mitatu ya kukamilisha mkataba wake wa sasa. (***Metro***)

### HAZARD KUREJEA UBELGIJI
BAADA ya kukamilisha uhamisho kutoka Borussia Dortmund kwenda Anderlecht, Thorgan Hazard amemtaka kaka yake Eden mwenye umri wa miaka 32, ambaye bado ni mchezaji huru baada ya kuondoka Real Madrid, kurejea Ubelgiji. (***Sport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG, SANCHO BADO KIZUNGUMKUTI

**MANCHESTER,** England

Kocha huyo asema kwa sasa si sehemu ya nyota walioko katika...

ERIK ten Hag amekiri kuna shaka iwapo, Jadon Sancho ana mustakabali ndani ya Manchester United.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anafanya mazoezi peke yake kufuatia mzozo wake hadharani na Ten Hag baada ya kufungwa mabao 3-1 na Arsenal kabla ya mapumziko ya mechi kimataifa.

Vyanzo vimeiambia ESPN Sancho hajaomba radhi kwa jukumu lake katika mzozo huo na akizungumza katika mkutano na wanahabari juzi, kocha huyo wa United alikataa kusema kama mchezaji huyo wa kimataifa wa England ataendelea kuwa sehemu ya mipango yake ya muda mrefu pale Old Trafford.

"Sijui," alisema Ten Hag, alipoulizwa kama Sancho ataichezea tena United.

"Ninaiandaa timu yangu kadri niwezavyo, naweka juhudi zangu zote kwa wachezaji wanaopatikana. Hayupo, hivyo kwa wakati huu, yeye sio muhimu, kwa sababu hawezi kuchangia."

**Sancho amefukuzwa kwenye mazoezi ya kikosi cha kwanza baada ya kupinga hadharani sababu za Ten Hag kumtoa kuelekea mchezo wa Arsenal.**

Ten Hag alisema ni kwa sababu ya uchezaji duni wa mazoezi, kabla ya Sancho kutoa chapisho kwenye mitandao ya kijamii kusema maoni hayo "si ya kweli kabisa" na "nimefanywa mbuzi wa kafara kwa muda mrefu."

"Kwa mashabiki ni mazungumzo, nanyi vyombo vya habari ni mazungumzo, lakini kwa wachezaji sio mazungumzo," aliongeza.

"Wanataka kufanya vizuri. Kwa wachezaji ambao hawakuwa na nafasi nyingi, wanapata nafasi, kwa hiyo hii ni nafasi yao ya kuingia kwenye timu.

"Kwa hiyo, kama nilivyosema, tulikuwa na roho nzuri, kila mtu anaangazia mchezo huu na michezo ijayo."

Kwa sasa Sancho anafanya mazoezi peke yake.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI

EVERTON
VERSUS
ARSENAL

1 | 5.46
X | 4.29
2 | 1.58

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARTETA ASEMA JESUS ALIIBADILISHA ARSENAL

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema Gabriel Jesus "alibadilisha ulimwengu wetu" baada ya kujiunga na klabu hiyo kutoka Manchester City msimu uliopita wa joto na kumuunga mkono mshambuliaji huyo kurudi upya kwenye kiwango chake bora.

Jesus alitua hapo kwa dili la pauni milioni 45 na kufufua safu ya ushambuliaji ya washikabunduki walipoanzisha changamoto ya ubingwa bila kutarajiwa kabla ya kumaliza kwa pointi tano nyuma ya mabingwa watetezi, City.

Jesus alipata jeraha la goti Desemba, mwaka jana alipokuwa akiichezea Brazil kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar ambalo lilimweka nje kwa zaidi ya miezi mitatu na kuanza kwake kampeni za 2023/24 kwa kucheleweshwa baada ya kufanyiwa upasuaji wa pili mdogo.

Hata hivyo, alifunga bao akitokea benchi katika ushindi wa magoli 3-1 wa Arsenal dhidi ya Manchester United kabla ya mapumziko ya kimataifa, goli lake la 12 katika mechi 35 alizoichezea klabu hiyo.

"Ukiangalia miezi sita au saba iliyopita kwa Gabi, pamoja na jeraha la muda mrefu alilokuwa nalo na kiasi cha soka alichokosa, basi alirejea katika maandalizi ya msimu mpya na akaanza kupata mdundo wake tena, na kisha alikuwa na jeraha lingine, upasuaji mwingine," alisema Arteta.

"Kwa hiyo tunapaswa kumjenga. Ni mchezaji mzuri sana, mchezaji muhimu sana kwetu. Alibadilisha ulimwengu wetu msimu uliopita. Mnaweza kuona hilo. Atakuwa mchezaji muhimu sana kwetu.

# Ndondo Cup Shinyanga yaiva

**NA SHABAN NJIA,** KAHAMA

TIMU 16 zimethibitisha kushiriki katika mashindano ya ndondo (Clouds Ndondo Cup 2023), yatakayofanyika kuanzia Oktoba Mosi, mwaka huu katika mkoa wa Shinyanga, imeelezwa.

Bingwa wa mashindano hayo mwaka huu atapata Sh. milioni tano na mshindi wa pili Sh. milioni tatu.

Mratibu wa mashindano hayo, Yahya Mohamed, alisema michuano hiyo inafanyika kwa ushirikiano na viongozi wa Chama cha Soka Mkoa wa Shinyanga (SHIREFA), pamoja na cha Wilaya ya Kahama (KDFA).

Alisema pia kutakuwa na zawadi ya mchezaji bora, kipa bora, kiungo bora na mfugaji bora, ambapo kila mmoja ataondoka na Sh. 300,000 huku kikundi bora cha kutoa hamasa kitajipatia Sh. 500,000.

Mwenyekiti wa KDFA, Salum Hussein alisema fursa ya kufanyika kwa mashindano hayo imefika katika muda mwafaka na wanaamini wachezaji wataonyesha vipaji vyao mbele ya makocha wa timu kubwa ambazo zinatarajiwa kwenda kusaka nyota wapya.

Naye Shamba Simon, akizungumza kwa niamba ya makocha, alisema Kahama ina wachezaji wenye vipaji na amewaomba waandaaji kujiepusha na vitendo vya upangaji matokeo.

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Vijana wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa JKM Park ili kujiandaa na mashindano mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TCB YAIBEBA WIZARA YA MAJI KUELEKEA SHIMIWI

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TIMU ya netiboli ya Wizara ya Maji imekabidhiwa vifaa vya michezo na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yatakayoanza hivi karibuni.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 1.4, Meneja wa Kanda wa TCB, Shaban Telatela alisema wametoa vifaa hivyo ili kuunga jitihada za serikali za kuimarisha michezo katika wizara na idara zake hapa nchini.

Telatela alitaja baadhi ya vifaa ambavyo TCB wamekabidhi ni pamoja na mipira na jezi zitakazotumika wakati wote wa mashindano.

Alisema anaamini wachezaji wa timu hiyo wanaendelea kujifua kwa ajili ya kujiweka imara kuelekea michuano hiyo ambayo ina ushindani katika kila mchezo. "Tumeamua kutoa vifaa vya michezo kwa timu hii kama moja ya kuthamini michezo, tunafahamu michezo ni afya kwa jamii hivyo tunapaswa kushiriki ili kuimarisha afya zetu", alisema Telatela.

Alisema wanaamini upatikanaji wa vifaa hivyo utakuwa ni moja kati ya chachu ya kuimarisha sekta ya michezo nchini hususani kwa wafanyakazi ambao timu zao zinashiriki katika michezo mbalimbali.

"Hii timu ni wadau wetu na tumekuwa tukishirikiana katika mambo mbalimbali ndio maana tumetoa vifaa ili kuongeza hamasa kwa wachezaji," alisema Telatela.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Rasiliamali Watu wa Wizara ya Maji, Wanyendo Kutta alisema wamefurahi kupokea vifaa hivyo vya michezo na anaamini vitawasidia katika kufikia malengo.

"Tunashukuru sana, tumepokea vifaa hivi vya michezo kutoka kwa wenzetu wa TCB, inaonyesha dhahiri kuunga mkono jitihada za rais wetu katika kuboresha, kuimarisha na kuendeleza michezo nchini" alisema Kutta.

Michezo ya SHIMIWI mwaka huu itafanyika mkoani Iringa na itashirikisha michezo ya soka, netiboli na kuvuta kamba kwa wanawake na wanaume.

# *Yanga yatakata, Simba yashikwa*

INATOKA UK. 24

ingia moja kwa moja katika nyavu za Wekundu wa Msimbazi.

Wenyeji walienda mapumziko wakiwa mbele kwa bao 1-0, licha ya kila upande kufanya mashambulizi ya mara kwa mara.

Dakika ya 59 Chama aliisawazishia Simba kufuatia kipa wa Power Dynamos kutema shuti lililopigwa na Mzamiru Yassin aliyepokea pasi nzuri kutoka kwa Mkongomani Jean Baleke.

Mabadiliko yaliyofanywa na Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' yalisaidia kuzaa matunda baada ya kusawazisha lakini Baleke na Saido Ntibazonkiza walionekana hatari katika lango la Power Dynamos.

Power Dynamos waliendelea kuwa 'moto' na kufunga bao la pili dakika ya 74 kupitia kwa, Cephas Mulombwa aliyepiga shuti la mbali ambalo lilimshinda kipa mpya wa Simba, Ayoub Lakred na mpira kutinga wavuni.

Chama alidhihirisha ni 'Mwamba wa Lusaka' kwa kuisawazishia Simba kwa mara ya pili kwa kupiga shuti la mbali ambalo lilimshinda kipa wa Power Dynamos kudaka.

Dakika ya 65 Ntibazonkiza alikosa nafasi ya wazi kwa kupiga shuti pembeni baada ya kupokea pasi kutoka kwa Kibu Denis huku Baleke akiwanyima furaha Simba kwa kushindwa kufunga katika nafasi zaidi ya tatu alizopata.

# Singida FG, Future kibaruani

INATOKA UK. 24

kucheza kwa kiwango cha juu kwa sababu wanahitaji ushindi na si matokeo mengine.

Nyota huyo alisema wanajua hakuna mechi rahisi, hivyo wamejipanga kukutana na ushindani kutoka kwa wapinzani wao.

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 17/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 2551 | PEC Zwolle vs GO Ahead Eagles | 2.31 | 3.31 | 2.82 |
| 13:30 | 4094 | Cagliari vs Udinese | 2.82 | 3.28 | 2.56 |
| 14:00 | 4849 | Millwall vs Leeds | 2.87 | 3.27 | 2.30 |
| 14:00 | 5000 | Lorient vs Monaco | 3.96 | 3.85 | 1.86 |
| 14:30 | 2391 | Eupen vs Standard Liege | 2.89 | 3.33 | 2.28 |
| 15:00 | 1262 | Getafe vs Osasuna | 2.58 | 2.94 | 3.10 |
| 15:00 | 1712 | Gor Mahia vs Nairobi City Stars FC | 1.38 | 4.21 | 7.21 |
| 15:00 | 1998 | FC Talanta vs Muranga Seal | 2.20 | 3.00 | 3.20 |
| 15:30 | 5386 | Bahir Dar Kenema FC vs Africain | 3.82 | 2.87 | 2.00 |
| 16:00 | 1232 | Strasbourg vs Montpellier | 2.34 | 3.55 | 2.93 |
| 16:00 | 1519 | Frosinone vs Sassuolo | 2.83 | 3.45 | 2.46 |
| 16:00 | 3414 | Clermont Foot vs Nantes | 2.01 | 3.55 | 3.70 |
| 16:00 | 3884 | Reims vs Brest | 1.89 | 3.69 | 4.00 |
| 16:00 | 4458 | Bournemouth vs Chelsea | 3.96 | 3.81 | 1.87 |
| 16:00 | 4940 | Monza vs Lecce | 2.15 | 3.39 | 3.45 |
| 16:30 | 5463 | Heidenheim vs Werder Bremen | 2.36 | 3.82 | 2.74 |
| 17:00 | 2109 | Istanbulspor vs Basaksehir | 3.00 | 3.25 | 2.25 |
| 17:00 | 3063 | Fenerbahce vs Antalyaspor | 1.38 | 4.65 | 6.81 |
| 17:00 | 4124 | Kabwe Warriors vs Napsa Stars | 2.28 | 2.73 | 3.29 |
| 17:15 | 2297 | Villarreal vs Almeria | 1.48 | 4.75 | 6.19 |
| 17:30 | 1642 | FC Arouca vs Casa Pia Atletico | 2.28 | 3.19 | 2.99 |
| 17:30 | 3603 | ES Metlaoui vs CS Sfaxien | 3.07 | 2.77 | 2.36 |
| 17:30 | 4559 | Gil Vicente vs GD Estoril | 2.10 | 3.44 | 3.14 |
| 17:45 | 2472 | AZ Alkmaar vs Sparta Rotterdam | 1.49 | 4.16 | 5.54 |
| 18:05 | 2641 | Marseille vs Toulouse | 1.49 | 4.71 | 5.94 |
| 18:30 | 1392 | SV Darmstadt vs Monchengladbach | 2.93 | 3.55 | 2.34 |
| 18:30 | 2937 | BK Hacken vs Halmstads BK | 1.27 | 5.25 | 7.47 |
| 18:30 | 4936 | Elfsborg vs Kalmar | 1.37 | 4.46 | 6.48 |
| 18:30 | 5182 | Everton vs Arsenal | 5.46 | 4.29 | 1.58 |
| 18:30 | 5713 | Amazulu vs Cape Town City | 2.68 | 3.04 | 2.58 |
| 19:00 | 1267 | Fiorentina vs Atalanta | 2.48 | 3.50 | 2.78 |
| 19:00 | 1404 | Lokomotiv Moscow vs Gazovik Orenburg | 1.86 | 3.70 | 3.55 |
| 19:00 | 2539 | Aarhus vs Brondby | 2.33 | 3.18 | 3.02 |
| 19:30 | 3556 | Bnei Sakhnin vs Hapoel Katamon | 2.82 | 2.97 | 2.39 |
| 19:30 | 4123 | Sevilla FC vs Las Palmas UD | 1.66 | 3.82 | 5.37 |
| 19:30 | 5578 | OH Leuven vs KAA Gent | 4.06 | 3.77 | 1.74 |
| 20:00 | 2817 | Vitoria Guimaraes vs Portimonense | 1.54 | 3.92 | 5.56 |
| 20:00 | 4853 | Alanyaspor vs Kasimpasa | 2.09 | 3.46 | 3.15 |
| 20:00 | 4875 | Trabzonspor vs Besiktas | 2.90 | 3.42 | 2.24 |
| 20:15 | 1296 | St Truiden vs Mechelen | 2.32 | 3.33 | 2.83 |
| 20:15 | 2905 | Valerenga vs Aalesunds | 1.46 | 4.44 | 5.78 |
| 20:30 | 2478 | PAOK vs Aris Salonica | 1.55 | 3.70 | 6.25 |
| 20:30 | 4143 | Radnicki Nis vs FK Imt Novi Beograd | 1.75 | 3.32 | 4.22 |
| 20:35 | 1350 | Partizan vs Radnik Surduluca | 1.31 | 4.53 | 8.05 |
| 21:30 | 4550 | AEK Athens vs Olympiakos | 2.16 | 3.29 | 3.24 |
| 21:45 | 5455 | Roma vs Empoli | 1.44 | 4.51 | 7.37 |
| 21:45 | 5975 | Lyon vs Le Havre | 1.70 | 4.05 | 4.62 |
| 22:00 | 2955 | Real Madrid vs Real Sociedad | 1.74 | 3.79 | 4.73 |
| 22:30 | 2966 | Sporting Lisbon vs Moreirense | 1.22 | 5.79 | 10.98 |
| 23:30 | 1481 | Ittihad Tanger vs Mouloudia Oujda | 1.78 | 3.15 | 4.10 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Septemba 17, 2023

Nipashe




## Arteta: Jesus aliibadilisha Arsenal

UK. 22




Mshambuliaji wa Yanga, Stephanie Aziz Ki (katikati), akijipanga kuwatoka mabeki wa Al Merrikh katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Pele Kigali, Rwanda jana. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Singida FG, Future kibaruani

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Singida Fountain Gate wanatarajia kuwakaribisha Future FC kutoka Misri mchezo utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mchezo huo wa kwanza wa hatua ya pili katika michuano hiyo ya kimataifa utachezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate, Ernest Middendorp ambaye hii itakuwa mechi yake ya kwanza tangu alipokabidhiwa majukumu ya kukinoa kikosi cha timu hiyo alisema wamejipanga kupambana kwa sababu wanajua mchezo utakuwa mgumu.

Middendorp alisema wachezaji wake wako tayari kuonyesha kiwango cha juu ili wafikie malengo ya kupata matokeo chanya katika mechi hiyo na kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele.

"Maandalizi ya kikosi changu yanaendelea vizuri, wachezaji wangu pia wako tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi katika mchezo huo," alisema kocha huyo.

Aliongeza amewaangalia wapinzani wao na kufahamu ubora na madhaifu yao hivyo wataingia uwanjani wakicheza kwa tahadhari na kusaka matokeo mazuri wakitumia uwanja wa nyumbani.

"Maandalizi yamefanyika vizuri hakuna majeruhi, tutaingia uwanjani kwa tahadhari na kuwaheshimu wapinzani wetu, Future FC ni timu nzuri na wanauzoefu katika mashindano haya, mipango yetu ni kushinda nyumbani na kwenda ugenini kumaliza mechi,"Middendorp alisema.

Nahodha wa timu hiyo, Gadiel Michael, alisema wachezaji wamejiandaa

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yatakata, Simba yashikwa

## ●●● Mabao ya Musonda, Mzize yawapa kicheko Jangwani, Chama akiibeba...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

YANGA imeendeleza rekodi yake ya msimu uliopita ya kufanya vizuri ugenini baada ya kuichapa Al Merrikh mabao 2-0 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati watani zao, Simba wakivutwa sharubu na Power Dynamos katika mchezo mwingine wa michuano hiyo uliomalizika kwa sare ya mabao 2-2.

**Yanga iliyokuwa Kigali, Rwanda imejiweka katika nafasi nzuri ya kutinga hatua ya makundi huku Simba ambayo pia ilikuwa ugenini Zambia ikitakiwa kupambana kusaka matokeo bora itakapowaalika wapinzani wao.**

Mabao ya Mzambia Kennedy Musonda na Clement Mzize ndio yaliwapa furaha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara katika mchezo wa kwanza wa hatua ya kwanza uliochezwa kwenye Uwanja wa Pele Kigali.

Nje ya uwanja mashabiki wa Yanga ndiyo waliotawala zaidi majukwaani wakiwazidi wenyeji Al Merrikh iliyoamua kutumia uwanja huo kutokana na ghasia za kisiasa zilizoko nchini kwao, na ndani ya uwanja wakitawala mchezo kwa asilimia kubwa zaidi.

Wawakilishi hao wa Tanzania walilazimika kusubiri hadi dakika ya 60 kuweza kupata bao la kuongoza kutoka kwa mtokea benchi, Musonda aliyeingia kuchukua nafasi ya Mudathir Yahaya ambaye alifunga kwa kichwa akiunganisha faulo iliyopigwa na Pacome Zouzoua.

Alipiga faulo ya kiufundi juu ambayo pamoja na kuruka juu, mabeki wa Al Merrikh waliikosa, mfungaji aliruka juu na kuupiga kichwa kubadilisha mwelekeo uliomfanya kipa, Mohamed Mustapha aliyeruka, kuukosa mpira huo.

Dakika 18 baadaye, Mzize ambaye alikosa mabao mengi katika mechi hiyo, alipachika bao la pili lililoiweka Yanga karibu zaidi ya kutinga hatua ya makundi, Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya miaka 24 kupita.

Ngoma ilianzia kwa Pacome ambaye aliipeleka kwa Aucho, akampenyezea Stephane Aziz Ki, aliyeipiga kwa kisigino kwa mfungaji naye akaitendea haki kwa kumpeleka Mustapha pale pale alipopiga Musonda, mpira ukajaa kwenye kamba.

Ili kutinga hatua ya makundi, vijana hao wa Miguel Gamondi wanatakiwa ushindi au sare yoyote, lakini pia wasiruhusu mabao zaidi ya mawili watakaporudiana wiki ijayo kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Pambano lilianza kwa kasi na dakika ya tano tu, Yanga ilianza kuwasalimia wenyeji wao kwa Zouzoua kuondoka na mpira kwa kasi, akiwazidi mbio mabeki na kupiga krosi safi iliyopita mbele ya lango, lakini ikakosa muunganishaji.

Maxi Nzengeli alikosa bao la wazi dakika moja baadaye alipokuwa ndani ya eneo la hatari kutokana na kizaazaa kilichotokea langoni kwa Wasudan hao na krosi ya Mzize kumfikia miguuni, lakini shuti lake dhaifu liliishia katika mikono ya Mustapha.

Al Merrikh ilifika langoni mwa Yanga dakika ya 11 ilipofanya shambulizi kali, lakini kabla ya kiungo Brayan Angulo kupiga shuti, beki Mzanzibar, Ibrahim Hamad 'Bacca' alimwahi na kuuokoa hatari hiyo.

Nzengeli aliyekuwa akihaha huku na huko, aliupata mpira katikati ya uwanja na kuanza kupasua safu ya mabeki wa Al Merrikh, lakini shuti lake la dakika ya 14 liliwababatiza na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Baada ya kufungwa mabao mawili, Al Merrikh walionekana sasa kutoka nyuma na kuanza kushambulia, lakini wachezaji wao wakiongozwa na straika, Mohamed Alrasheed hawakuwa makini walipokaribia katika lango la Yanga.

Huko Zambia, Power Dynamos ndio ilikuwa ya kwanza kupata bao dakika ya 28 kupitia kwa mshambuliaji wake, Joshua Mitale baada ya kupiga krosi na mpira

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >